JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA WIZARA KUANZIA DESEMBA 2005 HADI MACHI 2009

Aprili, 2009

Utangulizi

Dira na Makusudio
Dira ya Wizara ni kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi. Aidha, makusudio ya wizara ni kutoa huduma muhimu za afya zenye uwiano wa kijiografia, viwango vya ubora unaokubalika, gharama nafuu na zilizo endelevu.

Madhumuni
Madhumuni ya wizara ni kuinua hali ya afya ya wananchi wote na hasa wale walioko kwenye hatari zaidi, kwa kuweka mfumo wa huduma za afya unaokidhi mahitaji ya wananchi.

Madhumuni Mahususi:

i. Kupunguza magonjwa na vifo, ili kuongeza umri wa kuishi wa watanzania wote kwa kutoa huduma bora za afya, pamoja na kuzingatia mahitaji ya makundi maalum, hususan; watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano, watoto walio katika umri wa kuanza shule na walio shuleni, vijana, watu wenye ulemavu, wanawake walio katika umri wa uzazi na wazee.

ii. Kuhakikisha kuwa huduma za afya ya msingi zinapatikana na kutolewa na mfumo madhubuti na kushirikisha jamii, kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo.

iii. Kukinga na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza, hususan; Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, magonjwa yatokanayo na lishe duni, afya ya mazingira, na sehemu za kazini na usimamizi wa kemikali.

iv. Kuhamasisha wananchi kuhusu maradhi yanayoweza kuzuilika, ili waweze kuyatambua na kutafuta mbinu za kuyadhibiti.

v. Kumuelimisha kila mwananchi, aelewe kuwa anawajibika moja kwa moja kutunza afya yake na ile ya familia yake.

vi. Kujenga ushirikiano kati ya sekta ya umma, sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kijamii na jamii katika kutoa huduma za afya.

vii. Kupanga, kutoa mafunzo na kuongeza idadi ya wataalam wa afya, wenye taaluma inayokidhi viwango kwa kuzingatia usawa wa kijinsia ili kutoa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote.

viii. Kuainisha, kukarabati miundombinu kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu, na kuweka mfumo wa kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya, vifaa na vitendea kazi.

ix. Kufanya mapitio na kutathmini Sera ya Afya, Miongozo, Sheria na viwango vya utoaji huduma za afya.

Majukumu ya Wizara

Majukumu ya Wizara ni pamoja na kuandaa na kusimamia Sera ya Afya na Ustawi wa Jamii na kutoa huduma za kinga na tiba, udhibiti wa kemikali na kuendesha uchunguzi wa kisayansi wa magonjwa na sababu za vifo, kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vipodozi na chakula; kusimamia, kudhibiti na kuendeleza huduma za tiba ya asili na mbadala; kusimamia huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto; kufanya ukaguzi wa huduma za afya zitolewazo katika ngazi mbalimbali; kuandaa, kusimamia, kuboresha utendaji wa kazi na kuongeza upatikanaji wa wataalamu wa afya na ustawi wa jamii.

Aidha, Wizara inaratibu na kusimamia masuala ya lishe nchini, kufanya utafiti wa magonjwa ya binadamu na kutumia matokeo kwa manufaa ya wananchi, kulinda haki za makundi maalum ambayo ni watu wenye ulemavu, watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi, wazee wasiojiweza na watoto walio katika mkinzano wa sheria na kushiriki katika kutoa huduma za dharura wakati wa maafa pamoja na kujiandaa kwa majanga. Pia, Wizara ina jukumu la kushiriki katika juhudi za kimataifa za kuimarisha huduma za afya kwa kuwa mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kimataifa zinazojishugulisha na huduma za afya.

Huduma za afya nchini zinatolewa kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na mabadiliko endelevu yanayofanyika katika sekta ya afya kwa lengo la kuleta uwiano katika upatikanaji wa huduma bora za afya mjini na vijijini. Katika kipindi cha kuanzia Desemba 2005 hadi Machi 2009, huduma zinatolewa kwa kuzingatia Sera, Dira, Dhamira na Mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama vile MKUKUTA, Mkakati wa Kitaifa 2025, Malengo ya Maendeleo ya Millennia na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 – 2010.

Utekelezaji wa Majukumu

Katika kipindi hicho, Mheshimiwa Waziri alihudhuria mikutano ya kimataifa ifuatayo:-

i. Mkutano wa kimataifa wa malaria nchini Marekani ambapo alikutana na Bill Gates na Mkewe Mellinda Gates kukubali kusadia Tanzania katika mpango wa udhibiti wa malaria. Aidha, asasi ya kimataifa ya MACEPHA kusaidia Afrika ikiwemo Tanzania katika ufuatiliaji wa udhibiti wa malaria.

ii. Mkutano maalum wa Umoja wa Mataifa uliotambua mafanikio makubwa kutokana na juhudi za uongozi wa juu wa serikali akiwemo Mhe. Rais katika suala la upimaji wa hiari wa virusi vya UKIMWI nchini, ambapo watu zaidi ya milioni nne walipimwa.

iii. Mkutano wa SADC uliofanyika mjini Durban Afrika Kusini, Mh. Waziri alifanikiwa kushawishi wajumbe kuwa na sauti moja katika mpango wa udhibiti wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele (Neglected Tropical Diseases) kama vile Usubi (Onchocerciacis), Vikope (Trachoma), Matende na Ngirimaji kwa ajili ya kuongeza raslimali zaidi za kudhibiti magonjwa haya.

Aidha, Mheshimiwa Waziri alifanya ziara nchini Cuba na kufanikiwa kupata nafasi 20 za masomo ya udaktari kwa gharama ya nchi hiyo. Pia, Serikali ya Cuba imekubali kuleta madaktari nchini ili kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa madaktari. Vile vile alifanya ziara nchini Italia na ambapo Serikali hiyo imekubali kugharamia huduma za tiba ya saratani katika Hospitali ya Rufaa Bugando.

Utawala na Utumishi

Ajira za Watumishi wa Kada za Afya

Katika kipindi cha Desemba, 2005 hadi Machi 2009 jumla ya watumishi 11,709 wa kada mbalimbali za Afya wakiwemo Madaktari, Wauguzi, Mafundi sanifu, Wazoeza Viungo, Maafisa Wauguzi, Wafamasia, Wahudumu wa Afya, Tabibu na Makatibu wa Afya wamepangiwa kufanyakazi katika Sekretarieti za Mikoa yote, Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji, na Wilaya zote na katika baadhi ya Wizara. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 67 ya vibali vyenye wataalamu 17,245 vilivyotolewa katika kipindi hicho. Idadi hiyo ya kuwapangia wahitimu wa kada za afya imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kama inavyoonyesha hapo chini:-

MWAKA	KIBALI KILICHOTOLEWA	IDADI YA WATAALAMU WALIOPANGIWA VITUO VYA KAZI
2005/2006	1,677	983
2006/2007	3,890	3,669
2007/2008	6,437	4,812
2008/2009	5,241	2245 na zoezi la kuwapangia vituo vya kazi linaendelea.

Mishahara ya Watumishi wa Kada za Afya

Katika kipindi cha 2006-2008, Mishahara ya Watumishi wa Sekta ya Afya imeboreshwa. Kwa sasa watumishi wa kada za afya ndiyo wanaolipwa mishahara mikubwa ikilinganishwa na watumishi wa kada nyingine katika Utumishi wa Umma. Hali hii imewavutia watu waliosomea fani mbalimbali za Afya kuingia kwenye Utumishi wa Umma.

Mishahara ya watumishi wa mashirika ya dini na yasiyokuwa ya kiserikali
Wizara inalipa mishahara ya watumishi wa afya katika vituo vya kutolea huduma za afya vya mashirika ya dini na yasiyokuwa ya kiserikali yanayotoa huduma bila faida. Hospitali zinazopewa fedha ni Hospitali Teule 25 na Mashirika yasiyo ya Kiserikali 96. Aidha, hospitali Teule ya mkoa wa Dar Es Salaam imeanza kulipwa mishahara baada ya kukamilisha mchakato wa kuwekeana saini mkataba wa makubaliano (Memorandum of Understanding) kati yao na Serikali.





Kupanda kwa Mshahara

Upandishwaji Vyeo
Katika kipindi cha 2006-2008 wizara imewapandisha vyeo jumla ya watumishi 2,061 ambao wapo chini ya mamlaka ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Kada za Afya
Wizara imefanya marekebisho ya Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Kada za Afya ili kujumuisha baadhi ya kada ambazo awali hazikuwa kwenye muundo huo kama vile Maafisa Wauguzi, Maafisa Afya na Wazoeza Viungo ngazi ya Shahada, kutenganisha sifa za Madaktari wa Kawaida na Madaktari Bingwa, kujumuisha kada mpya za matabibu wasaidizi, wasaidizi wa maabara, maafisa afya wasaidizi n.k. zilizoanzishwa ili kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ambao unalenga kuwa na Zahanati katika kila kijiji na Vituo vya afya kwa kila kata.

Aidha, katika Muundo huo umeongezwa kada ya Maafisa Lishe ambayo imeanzishwa ili kukabilina na tatizo la lishe nchini ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari na magonjwa ya moyo.

Taratibu za Uendeshaji wa Huduma za Afya
Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Wizara imeandaa taratibu za Uendeshaji wa huduma za afya nchini. Taratibu hizi zimeundwa ili kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini

Muundo wa Wizara (Organization Structure)
Kufuatia mabadiliko ya Wizara yaliyofanywa mwaka 2006 kwa kuiunganisha Wizara ya Afya na Idara ya Ustawi wa Jamii; Wizara ililazimika kubadili Muundo wake ili kuendana na mabadiliko husika. Hivi sasa Muundo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Organization Structure) tayari umekamilika na kupitishwa.

Ofisi ya Malalamiko
Wizara imeanzisha Ofisi ya Maalum ya kushughulikia malalamiko yanayohusiana na mwenendo mzima wa utoaji na upatikanaji wa huduma za afya nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa malalamiko yanafanyiwa kazi pale yanapotokea. Tangu ofisi ilipofunguliwa Julai, 2007 mpaka sasa Wizara imepokea jumla ya malalamiko 117. Malamiko 92 tayari yamefanyiwa kazi kwa kupatiwa ufumbuzi. Aidha, malalamiko 25 yanaendelea kufanyiwa kazi.

Baraza la Majadiliano ya Pamoja Katika Sekta ya Afya (Health Service Joint Staff Council)
Baraza hili pamoja na mabaraza mengine ya kisekta limeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Na. 19/2003. Baraza lilizinduliwa tarehe 6 Oktoba, 2008.

Majukumu ya Baraza ni pamoja na:-

i. Kutoa ushauri kwa Serikali katika masuala yanayohusu ustawi wa watumishi wa sekta.
ii. Kujadili na kutoa maoni kwa serikali kuhusu masuala yanayohusu ustawi na ufanisi wa watumishi.
iii. Kujadili masuala yanayohusu masharti ya kazi ya watumishi kwa ujumla au utaratibu wa huduma katika sekta
iv. Kujadili masuala yoyote yaliyopelekwa na Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma.

Huduma za Usafirishaji
Wizara imetoa mwongozo wa kuendesha, kusimamia na kudhibiti mfumo wa usafirishaji katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini. Kupunguza gharama za matengenezo na kuongeza uhai wa magari katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

Mradi wa Ajira za Dharura (Emergency Hiring Project)
Wizara kwa kushirikana na Mkapa Fellows Programme imeajiri watumishi 99 katika halmashauri 33 Tanzania Bara na Zanzibar. Chini ya Programu hii watumishi walioajiriwa ni Madaktari, Wafamasia, Wauguzi na Wataalam wa Maabara. Halmashauri zilizonufaika na Programu hii ni Serengeti, Tarime, Bunda, Meatu, Bukombe, Sikonge, Urambo, Igunga, Iramba, Manyoni, Singida Vijijini, Nkasi, Mpanda, Sumbawanga Vijijini, Nachingwea, Kilwa, Ruangwa, Liwale, Tandahimba, Newala, Kilindi, Handeni, Simanjiro, Kiteto, Hanang, Kilolo, Njombe, Monduli, Makete, Kibondo, Kaskazini Unguja, Micheweni na Wete. Ajira ya watumishi hao inagharamiwa na Serikali ya Norway pamoja na Clinton HIV/AIDS Foundation.

Kutokana na uzoefu uliopatikana katika halmashauri 33, Wizara kwa kushirikiana na Benjamini Mkapa Aids Foundation (BMAF) imeajiri watumishi 176 katika Halmashauri 19 chini ya “Emergency Hiring Project”. Halmashauri zilizonufaika na mradi huo ni Biharamulo, Kishapu, Mafia, Bagamoyo, Masasi, Pangani, Kilosa, Ulanga, Mufindi, Ludewa, Kyela, Mbozi, Ileje, Tunduru, Namtumbo, Hai, Ngorongoro, Mwanga na Nzega. Watumishi walioajiriwa ni Madaktari, Madaktari Wasaidizi, Tabibu, Wafamasia/Fundi Dawa Sanifu, Wauguzi, Fundi Maabara Sanifu na Maafisa Ustawi. Watumishi hao wanafanyakazi chini ya Mradi huo kwa muda wa miaka 3 na baada ya hapo wataajiriwa na Serikali na kubakia katika halmashauri hizo. Ajira ya watumishi hao inagharamiwa na Global Fund.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na miradi hiyo miwili ni pamoja na yafuatayo:
i. Kutambua maeneo ya mazingira magumu (underserved areas) na mfumo wa motisha (incentive package). Miradi hiyo imewezesha kubakiza watumishi kazini kwa zaidi ya asilimia 84.

ii. Kutoa mchango mkubwa Serikalini katika mchakato unaoendelea wa kutengeneza rasimu ya Taifa ya kutambua maeneo ya mazingira magumu na utengenezaji wa motisha kwa watumishi wote wa umma wakiwemo wa sekta ya afya; kazi ambayo bado inaendelea chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

iii. Watumishi walioajiriwa ni 275 kati ya hao asilimia 5 ni wastaafu.

iv. Wastani wa asilimia 50 ya watumishi walioajiriwa wameonyesha nia ya kuajiriwa katika Utumishi wa Umma. Aidha, watumishi 27 tayari wameajiriwa Serikalini mwaka wa fedha 2008/09. Wengine 90 wanatarajiwa kuajiriwa katika mwaka wa fedha 2009/10. Hali hii itasaidia kuziba pengo la upungufu wa watumishi katika Sekta ya Afya.

v. Kuimarisha uongozi katika idara za afya za halmashauri na kuziba upungufu wa Waganga Wakuu wa Wilaya wenye sifa, madaktari 8 waliokuwa chini ya mradi wa Mkapa Fellows Programme wameajiriwa na kuteuliwa kuwa Waganga Wakuu wa Wilaya.

vi. Huduma za UKIMWI katika Halmashauri hizo 52 zimeboreshwa.

Ajira chini ya miradi hii miwili ya Mkapa Fellows Programme na Emergency Hiring Project itafikia tamati mwaka 2010 na imeongeza idadi ya wagonjwa wanaopata huduma kama inavyoonyesha katika vipindi viwili tofauti hapa chini.





Sera Na Mipango

Sera na Mipango ni kiungo muhimu katika kusimamia na kuratibu Sera za Wizara, Uandaaji wa Mipango, Bajeti na uratibu wa shughuli za ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, inasimamia Mabadiliko katika Sekta ya Afya na Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji Huduma za Afya (MTUHA). Pia, inaratibu mahusiano ya Kimataifa, ikiwa ni pamoja na masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Nchi za Afrika (AU) na Mataifa mengineyo.

Wizara imeweka mazingira mazuri ya kuwawezesha Wadau mbalimbali wa Maendeleo wakiwemo wa Mfuko wa Pamoja (Basket Fund) na wengine wanaosaidia Maeneo Maalum ya Afya (Direct to Project Funds). Wizara inatayarisha Mikakati pamoja na Mipango mbalimbali kwa kuwashirikisha Wadau wote, kushirikiana katika hatua za utekelezaji, kufanya tathmini na kupima mafanikio kwa uwazi. Hali hii imeongeza imani kwa Wadau hao na kuwa chachu kwao ya kuongeza viwango vya fedha wanazotoa kwa Sekta ya Afya.

Sera ya Afya

Wizara imeandaa Sera mpya ya Afya kwa kupitia Sera ya mwaka 1990. Sera hii ilipitishwa mwaka 2007. Maboresho katika sera hii yanalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora karibu zaidi na wananchi, ushirikishwaji wananchi katika kupanga, kubuni mbinu mpya na kuchangia huduma za afya.

Maeneo muhimu yaliyoainishwa katika Sera ya Afya ya mwaka 2007

a) Huduma za afya ya msingi
b) Huduma za kinga ikiwemo huduma ya mama na mtoto
c) Huduma za tiba zikiwemo huduma za uchunguzi wa magonjwa, dawa, vifaa,vifaa tiba, vitendanishi, na tiba asili na mbadala.
d) Huduma za utengamao
e) Maendeleo ya Watumishi na Vyuo vya Mafunzo vya Sekta ya Afya.
f) Rasilimali

g) Mipango ya Afya
h) Huduma nyingine
i) Wakala na Taasisi zilizopo chini ya Wizara
j) Mabaraza na Vyama vya Kitaaluma
k) Masuala Mtambuka ya Sera
l) Muundo wa Kitaasisi
m) Mfumo wa Kisheria

Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM)
Wizara imeandaa mpango kabambe wa MMAM 2007-2017. Lengo la mpango huo ni kuongeza kasi ya kupeleka huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata na hospitali kila Wilaya. Hii ni pamoja na kukarabati na kuongeza majengo katika vyuo vya afya vilivyopo ili kuongeza idadi ya wanafunzi. Lengo ni kutoa wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kutoa huduma katika vituo hivyo. Aidha, katika mpango huo majukumu ya kila ngazi yameainishwa.

Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya
Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya 2009-2015 wenye lengo la kuongeza ufanisi na kasi katika utoaji wa huduma za afya. Wadau wote wamehusishwa wakiwemo Washirika wa Maendeleo. Mkakati unalenga ngazi zote za huduma kuanzia kaya, kata, wilaya, mkoa na taifa ili kuboresha upatikanaji wa rasilimali watu, fedha, vifaa na miundombinu.

Mabadiliko katika Sekta ya Afya
Mabadiliko ya Sekta ya Afya yanaendeshwa kwa mfumo wa majadiliano ya pamoja ya kisekta (Sector Wide Approaches-SWAP). Aidha, Wizara imeridhia utaratibu wa kutumia mpango huu pamoja na “Health Basket Fund” (HBF), na wengine kutumia miradi na Taasisi zisizo za Kiserikali -NGOs. Fedha hizo zote zinaingizwa kwenye Medium Term Expenditure Framework (MTEF).

Ushiriki katika kupima Mafanikio ya Serikali (GBS-PAF)
Serikali imeridhia mpango huu wa Maendeleo ikishirikiana na wadau wa maendeleo na sekta ya afya imeweza kushiriki vikao vyote kwa mafanikio. Mafanikio hayo yamewahamasisha wadau wa maendeleo kuendelea kutoa michango yao kupitia GBS/PAF na Basket Fund.

Serikali na Wadau wa Maendeleo
Kwa kushirikiana na wadau wa Mfuko wa Pamoja kumekuwa na ongezeko la fedha inayotengwa kutoka dola za Kimarekani 0.5 mwaka 2006 hadi dola moja kwa kila Mtanzania mwaka 2008. Fedha hizi zinapelekwa katika halmashauri wanakoishi wananchi wengi. Maamuzi ya matumizi ya fedha hizi hufanywa na halmashauri zenyewe kwa ajili ya kuboresha huduma za afya chini ya mfumo wa ugatuaji wa madaraka”D by D”.Mfumo huu umehamasisha wahisani kuingia basket funds kutoka watano (5) hadi kufikia 13.

Mchango wa wananchi katika Huduma za Afya
Wananchi wameshiriki katika michango mbalimbali kwa lengo la kuboresha huduma za afya nchini. Michango ya wananchi inapatikana kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na uchangiaji wa moja kwa moja (Cost Sharing). Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi waendelee kuchangia huduma za afya.

Mapitio ya Sekta ya Afya kwa pamoja na Wahisani ya kila mwaka
Sekta ya Afya imefanya mapitio ya utoaji huduma kwa miaka tisa mfululizo. Mapitio hayo yamesaidia kupima ufanisi wa sekta kiutekelezaji. Aidha, mapitio hayo yamefanya wadau kujenga imani na Serikali. Fedha zilizotolewa na Mfuko wa Pamoja (Health Basket Fund) mwaka wa fedha 2008/09 ni kiasi cha shilingi 96,145,100,040 ikilinganishwa na shilingi 56,400,000,000 mwaka wa fedha 2005/2006. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 70.

Tathmini ya Skta ya Aya
Tathimini ya miaka 6 kuanzia 1999 hadi 2006 ilifanyika mwaka 2007. Tathimini hiyo imebaini kwamba ubora wa huduma umeongezeka, vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 68 hadi 58 kati ya mwaka 2005 hadi 2008 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai. Aidha, ilibainika kuwa upatikanaji wa fedha umeongezeka hasa kupitia Health Basket Fund.

Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia
Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya kupunguza vifo vya mama na mtoto, kupunguza kasi ya maambukizi ya UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu. Vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja na miaka mitano vimepungua kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai:-

Umri	2005	2008
Watoto wachanga chini ya siku 28	32	29
Watoto chini ya mwaka mmoja	68	58
Watoto chini ya Miaka 5	112	91

Lengo la milenia ni kupunguza vifo hivyo vya watoto chini ya miaka mitano hadi asilimia 54 ifikapo mwaka 2015.

Huduma za Afya katika ngazi ya Halmashauri
Katika kutekeleza mpango wa serikali wa kupeleka madaraka na rasilimali katika ngazi ya Halmashauri, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI, yamefanyika yafuatayo:-

i. Kuandaa miongozo na mipango ya afya katika halmashauri

ii. Kuratibu na kutoa ushauri kuhusu Mipango Kabambe ya afya ya halmashauri

iii. Kuandaa miongozo ya mipango ya vituo vya afya na zahanati

iv. Kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa kupunguza vifo vya mama na mtoto katika halmashauri kwa kutoa motisha kwa wafanyakazi

Takwimu

Utafiti kuhusu upatikanaji wa huduma za afya (Service Availability Mapping Survey) ulifanyika katika mikoa na halmashauri. Takwimu zilizopatikana zimesaidia katika kupanga Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), uboreshaji wa Sera ya Afya na kupanga mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za afya. Utafiti huu umesaidia kujua ni sehemu zipi za nchi ambazo hazijafikiwa na huduma muhimu za kiafya kama vile vyandarua, dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, kifua kikuu, tiba ya malaria n.k

Wizara kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Takwimu, imefanya tafiti zifuatazo:

a) Huduma zitolewazo pamoja na ubora wake (Tanzania Service Provision Assessment Survey 2006).

b) Hali ya ugonjwa wa UKIMWI na malaria. Aidha utafiti huu pia ulifanywa kwa ushirikiano na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS)

Tafiti hizi zimesaidia kutoa viashiria mbalimbali vya MKUKUTA, malengo ya Milenia na mwenendo wa huduma zinazotolewa katika sekta ya afya. Aidha tafiti hizi zimesaidia kujua mwenendo mzima wa janga la UKIMWI hapa nchini jambo ambalo limesaidia kujipanga upya katika kukabiliana na janga hili.

Mafunzo ya utafiti kwa timu za uendeshaji wa Afya za wilaya na mikoa katika mikoa kumi (10) ya Tanzania bara yamefanyika, ambayo ni Mwanza, Kagera, Mara, Dodoma , Shinyanga, Ruvuma,Manyara,Mtwara, Lindi, na Kilimanjaro.

Tovuti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeunganishwa na tovuti zingine za taasisi zinahusiana na kutoa huduma za afya hapa nchini (www.moh.go.tz) ili kuboresha mawasiliano na upatikanaji wa taarifa.

Sheria

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kina jukumu la kupitia na kutoa ushauri kuhusu sheria mbalimbali zinazoandaliwa na Wizara pamoja na taasisi zake. Aidha, Será ya Afya ya 1990 ilifanyiwa mapitio na kupitishwa 2007 ili kukidhi mahitaji ya sasa. Kutokana na mabadiliko hayo, sheria zifuatazo zimeweza kuandaliwa na kupitishwa:

a) Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Maabara za Afya 2007
b) Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mionzi na Radiolojia 2007

c) Sheria ya Wataalam wa Macho 2007
d) Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya Ukimwi (VVU) 2008
e) Sheria ya Afya ya Akili 2008.
f) Sheria ya Afya ya Jamii 2008
g) Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuingiza wastaafu na Madiwani.

Aidha, Muswada wa Teknolojia ya DNA ya Binadamu unatarajiwa kujadiliwa katika mkutano wa 15 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili 2009. Pia, miswada mbalimbali ipo katika hatua za kuwasilisha nyaraka za Baraza la Mawaziri ya mapendekezo ya Sheria ya Huduma za Afya, Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Sheria ya Usimamizi wa Taaluma ya Uuguzi, Sheria ya Famasi na Sheria ya Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku.

Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali

Mganga Mkuu wa Serikali ana wajibu wa kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Waziri na Katibu Mkuu juu ya masuala yote yanayohusu taaluma ya afya. Aidha, ni msimamizi mkuu wa sera, uratibu na ufuatiliaji wa huduma za afya zikiwemo kinga, tiba ya magonjwa, mafunzo na maendeleo ya watumishi katika Sekta ya Afya, utengamao, huduma za dharura na maafa, huduma za uuguzi na ukunga, viwango vya ubora wa huduma na ukaguzi wa huduma za afya. Pia, ni msimamizi wa mabaraza ya kitaaluma na mshauri wa vyama vya kitaaluma.

Ukaguzi na Ufuatiliaji Ubora

Usimamizi na ukaguzi wa huduma za afya ulifanyika katika mikoa mitatu ikijumuisha Halmashauri sita za Arusha Manispaa, Monduli, Iringa Manispaa, Njombe, Kibaha na Rufiji. Ukaguzi ulifanyika katika hospitali 16, vituo vya afya 13, zahanati 41, maabara binafsi 8, maduka ya dawa moto 6 na maduka ya dawa baridi 13.

Mikutano miwili ya wadau ilifanyika kwa ajili ya kupitia mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Huduma za Afya (Health Services Bill).

Mafunzo ya kujikinga na kudhibiti maambukizi (Infection Prevention and Control) na uboreshaji wa huduma za afya (Quality Improvement in healthcare) yalitolewa kwa watoa huduma za afya 4,720 kutoka hospitali 33 (Hospitali za Rufaa za: Bugando, KCMC, Mbeya, Hospitali ya Taifa Muhimbili, na Hospitali ya Mnazi Mmoja ya Unguja, Hospitali za Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa, Morogoro, Dodoma, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Kigoma, Tabora, Mtwara, Lindi na Singida; Hospitali za Wilaya za Chake-Chake, Rufiji, Muleba (Rubya DDH), Korogwe, Kilombero (St. Francis Ifakara), Mpwapwa, Kinondoni, Ilala na Temeke; pamoja na Hospitali Maalumu ya Tumbi Kibaha.

Mwongozo wa kukinga na kudhibiti maambukizi kwa watoa Huduma za Afya (Pocket Guide) uliandaliwa. Aidha, Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Afya unaojulikana kama 5S- CQI-TQM unatekelezwa katika Hospitali ya Rufaa Mbeya, Hospitali ya Taifa Muhimbili, KCMC, Bugando, Maweni - Kigoma, Dodoma, Lindi, Mtwara, Newala, Masasi, Nachingwea na Tandahimba.

Dharura na Maafa

Timu ya Dharura ya Kitaifa (National Rapid Response Team) yenye wataalam 40 imeanzishwa. Timu hiyo imegawanyika katika makundi mawili, ya dharura zinazohitaji huduma za upasuaji (surgical cases) na dharura zinazohitaji huduma za tiba (medical cases).

Aidha, timu hizo zilishiriki katika kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa Rift Valley Fever (RVF) katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Morogoro, Iringa na Manyara mwishoni mwa mwaka 2006. Pia, timu hizi zilishiriki katika uokoaji na uhifadhi wa miili ya wachimbaji madini waliokufa kutokana na mafuriko katika migodi ya Mererani na Simanjiro, mkoani Manyara mwezi Februari 2008. Vilevile, timu hizo zilishiriki katika uchunguzi wa athari za kiafya zilizotokana na mlipuko wa Mlima wa Oldonyo Lengai mkoani Arusha mwaka 2008.

Wizara imetoa mafunzo maalum juu ya 'Mass Casualty Management' kwa Kamati za Uendeshaji Huduma za Afya katika mikoa yote 21. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa Mikoa juu ya kuzuia na kudhibiti ugonjwa wa Ebola na Marburg. Mikoa hiyo ni Kagera,Rukwa, Mbeya, Mwanza na Mara. Pia, Wizara imetoa vifaa tiba vya dharura pamoja na dawa katika hospitali za Tumbi,Morogoro na Dodoma kufuatia matukio ya ajali za barabarani mwaka 2006 na 2007 yaliyosababisha vifo na majeruhi wengi kulazwa katika hospitali hizo.

Huduma za Uuguzi na Ukunga

Wizara imetayarisha miongozo ya kuboresha utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga. Miongozo hiyo ni pamoja na Basic Nursing and Midwifery Procedure Manual, Minimum Standards for Nursing and Midwifery Practice, Tanzania Nursing and Midwifery Model of Practice, Minimum equipment and supplies required for nursing and midwifery procedures, Nurses and Midwives Guidelines and Protocols for Preventing HIV/AIDS from needle stick and sharps injuries in Tanzania na Standard Checklist for monitoring and supervising nursing and midwifery services in the country.

Aidha, Wizara imeandaa Mwongozo wa Maadili ya Uuguzi na Ukunga ili kuimarisha nidhamu na maadili ya taaluma. Pia,Wizara imetoa mafunzo ya uongozi na utafiti kwa Wauguzi Wakuu wa Mikoa na Wauguzi Wakuu wa Hospitali ili kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma katika mikoa na wilaya.

Mabaraza ya Kitaaluma

Baraza la Macho na Miwani
Sheria mpya “Optometry Act” 2007 ilipitishwa na Bunge. Aidha, Wizara kupitia Baraza la Macho na Miwani imeandaa na kuchapisha kitabu cha maadili na mwenendo wa utendaji kazi wa wataalam wa upimaji macho na miwani. Pia, Wizara imeandaa mtaala wa wataalamu wa upimaji macho na miwani.

Baraza la Wauguzi na Wakunga
Wizara kupitia Baraza la Wauguzi na Wakunga imehakiki vyeti vya wauguzi 22,000 nchini. Jumla ya vyeti 64 vilibainika kuwa ni vya kughushi na wahusika walichukuliwa hatua za kisheria. Leseni zilitolewa kwa Wauguzi 22,000 wa zamani na wapya. Aidha, Wizara imeanzisha mfumo wa taarifa za Wauguzi na Wakunga nchini (Data Bank), ili kurahisisha upatikanaji wa kumbukumbu sahihi.

Tuhuma 14 dhidi ya Wauguzi waliovunja maadili zilisikilizwa na kutolewa hukumu. Kati ya tuhuma hizo, wauguzi 10 walipatikana na hatia na kupewa adhabu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuonywa, kupewa karipio na kusimamishwa kazi kwa muda. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa Wauguzi Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa, Mikoa, Wilaya ili kuwajengea uwezo wa kusimamia maadili na utendaji kazi.

Pia, Wizara imeongeza vituo vya kufanyia mafunzo ya vitendo kwa Wauguzi na Wakunga kutoka vituo 4 hadi kufikia 25.

Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala
Wizara kupitia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala imeandaa kanuni na miongozo mbalimbali ya utoaji wa Tiba Asili na Tiba Mbadala zifuatazo:

i. Kanuni za usajili wa waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala pamoja na wasaidizi wao na vituo rasmi vya tiba asili na tiba mbadala.
ii. Kanuni zinazohusu maadili na utendaji wa taaluma ya tiba asili na tiba mbadala.
iii. Kanuni za usajili wa dawa za asili na tiba mbadala.
iv. Kanuni za kukusanya maduhuri (fees and charges) ya Baraza.
v. Kanuni za kuendesha Baraza (inquiry procedures)
vi. Mwongozo wa Vituo vya kutolea huduma za tiba asili na tiba mbadala (Standard guidelines of traditional and alternative health facilities in Tanzania Mainland).
vii. Mwongozo wa Usimamizi na Ukaguzi wa huduma tiba asili na tiba mbadala (National supervision guidelines for quality traditional and alternative health care services)
viii. Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Baraza.
ix. Mwongozo wa Kufundishia Urasimishaji wa tiba asili na tiba mbadala.
x. Maafisa Watendaji wa Kata katika mikoa ya Iringa na Pwani walielimishwa kuhusu sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala na jinsi Ofisi zao zinavyohusika na usajili wa Watoa huduma wa tiba asili.

Baraza la Famasi
Wizara kupitia Baraza la Famasi imeandaa kanuni za Usajili wa Wanataaluma wa Famasi kama ifuatavyo:

Mwaka	Wafamasia (Pharmacists)	Pharmaceutical Technicians	Pharmaceutical Assistants
2006	560	126	110
2007	674	386	331
2008	700	420	349

Aidha, Wizara kupitia Baraza la Famasia imeandaa Kanuni za Elimu na Mafunzo (Education and Training Regulations) kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa stashahada ya Famasi. Pia, imeandaa mitaala ya mafunzo ya kujiendeleza kazini kwa taaluma ya famasi. Vilevile, imeandaa Kanuni na Miongozo ya Taratibu za kuendesha mahojiano kwa watuhumiwa wanaokiuka Maadili na Miiko ya Taaluma ya Famasi.

Wizara kupitia Baraza la Famasi imehamasisha na kuelimisha wanataaluma na wadau wa taaluma ya Famasi. Aidha, vitabu vya Sheria, Kanuni na Miongozo ilisambazwa kwa walengwa. Pia, Wizara imeongeza vituo vya kufanyia mafunzo ya vitendo kutoka vituo 4 hadi kufikia 10.

Baraza la Madaktari Tanganyika
Wizara kupitia Baraza la Madaktari Tanganyika limeandaa kanuni za Maadili na Miiko ya Taaluma ya Udaktari. Aidha, Wizara imeandaa mfumo wa takwimu (Data Base) kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za Madaktari waliosajiliwa. Pia, Wizara imeongeza vituo vya mafunzo kwa vitendo kutoka 4 hadi 13 ili kuondoa mlundikano wa madaktari wanaosubiri kuanza mafunzo ya vitendo. Vituo vilivyoongezeka ni pamoja na Temeke, Amana, Mwananyamala, Dodoma, Bombo-Tanga, Mount Meru – Arusha, Selian – Arusha, Ifakara St. Fransic na Peramiho.

Wizara kupitia Baraza la Madaktari Tanganyika imesajili Madaktari kama ifuatavyo:

Mwaka	Madaktari Mafunzo Kwa Vitendo	Madaktari	Madaktari Wasaidizi
2006	262	4,143	1,633
2007	385		
2008	359		

Wizara kupitia Baraza la Madaktari Tanganyika imeandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Elimu ya kujiendeleza, Nidhamu ya Taaluma, Vigezo vya kusitisha Daktari kufanya kazi kutokana na kupoteza uwezo (Professional Impairement) na kuendesha mafunzo ya vitendo.

Baraza la Maabara
Sheria mpya, Na. 22 ya mwaka 2007 ya Usajili wa Wataalamu wa Maabara ilipitishwa na Bunge.

Baraza la Radiolojia
Sheria mpya, Na. 21 ya mwaka 2007 ya Usajili wa Wataalamu wa Radiolojia ilipitishwa na Bunge.

Huduma za Kinga
Wizara katika kipindi cha miaka mitatu imeendelea kuimarisha huduma zake katika nyanja za afya ya mazingira, huduma za mama na mtoto, kudhibiti magonjwa ya kuambukiza yakiwemo ya milipuko.

Huduma za Afya na Usafi wa Mazingira
Sheria ya Afya ya Jamii (Public Health Act), imepitishwa na Bunge Januari 2009. Aidha, Sheria ya Usajili wa Wataalamu wa Afya ya Mazingira (The Environmental Health Practitioners (Registration) Act, 2007) imepitishwa.

Mpango Mkakati wa Afya na Usafi wa Mazingira umeandaliwa. Nia ya mpango huu ni kuinua kiwango cha usafi wa mazingira nchini na kutekeleza malengo ya MKUKUTA na MILENIA na utasaidia kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na milipuko.

Miongozo na viwango vya kudhibiti taka kutoka katika hospitali imeandaliwa na kusambaza katika wilaya zote nchini. Hali hiyo imewezesha kuboresha mifumo kwa kujenga matanuru (incinerators) bora ya kuteketeza taka katika hospitali 11 za mikoa na 69 za wilaya.

Wizara imehamasisha wilaya kuanzisha vijiji bora vya makazi kila mkoa na wilaya, ambavyo vinazingatia makazi bora, ikiwemo ujenzi wa nyumba na vyoo bora, uhakika wa kupata maji safi na salama, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira viwanja vya makazi vilivyopimwa na vyenye huduma nyingine muhimu. Vijiji vitano vimeanza mpango huo ambavyo ni, Namalenga, Masasi, Chumwi, Musoma Vijijini, Mkowe, Sumbawanga Vijijini, Kitisi, Iringa Vijijini na Kitunda, Ilala.

Udhibiti na ufuatiliaji wa Magonjwa (Epidemiolojia)
Taarifa za magonjwa nane ya kuambukiza na mlipuko ya kila wiki (Kipindupindu, Tauni, Surua, Homa ya Uti wa Mgongo, Kichaa cha Mbwa, Kupooza kwa ghafla, lishe ya watoto chini ya umri wa miaka mitano na vifo vya akina mama wajawazito), zinapokelewa kutoka mikoa yote ya Tanzania bara na kutathiminiwa katika ngazi zote za utoaji huduma kwa lengo la kudhibiti na kupunguza athari na usambaaji wa magonjwa husika. Pia kutoa taarifa ya nchi ngazi ya kimataifa kulingana na mkataba wa utoaji taarifa, kupitia Shirika la Afya Duniani.

Wizara imefanya ufuatiliaji wa ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege ambapo vituo viwili vimeanzishwa katika wilaya ya Kibondo (Kigoma) na Mwananyamala (Dar Es Salaam). Sampuli huchukuliwa na kupelekwa kwenye maabara ya kitaifa kwa ajili ya uchunguzi wa vimelea vya ugonjwa huo.

Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya (NIMR, CDC, AFENET, MUHAS, WHO) imeanzisha mafunzo ya shahada ya uzamili katika fani ya Epidemiolojia na Maabara (Epidemiology and Laboratory Management). Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa wataalam wa afya ngazi ya Wilaya, kuhusu mbinu mpya za ufuatiliaji wa milipuko (Outbreak investigation and response). Mafunzo hayo yametolewa katika wilaya 70 za Tanzania Bara.

Magonjwa ya Kuambukiza

Magonjwa Makuu

Malaria

Mwongozo mpya wa kutibu ugonjwa wa Malaria kwa kutumia dawa ya mseto ya Artemether/Lumefantrine (ALu) umeanza kutumika katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Mfuko wa Dunia (Global Fund) kwa ajili ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria umetoa fedha kiasi cha dola za kimarekani 90.468 milioni kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya manunuzi ya dawa mseto na kuelimisha watoa huduma wote nchini. Dawa hizo zinatolewa katika vituo vya matibabu 4,921.

Wamiliki/aina ya kituo	Hospitali	Kituo cha Afya	Zahanati	Jumla
Serikali	89	346	3,550	3,985
Mashirika ya kujitolea	87	85	508	680
Mashirika ya Umma/Jeshi	8	12	236	256
Jumla	184	443	4,294	4,921

Kwa kushirikiana na sekta binafsi wanawake wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano kote nchini wanaohudhuria kliniki ya mama na mtoto wanapata chandarua chenye viuatilifu kwa bei nafuu, kwa Mpango wa Hati Punguzo. Hadi mwezi wa Novemba 2008, zaidi ya akina mama wajawazito milioni tatu kati ya makadirio ya walengwa milioni nne na laki nane wamepata vyandarua vyenye uatilifu kwa kupitia mpango huu.

Kubuni, kuandaa na kuanza kutekeleza mpango maalum wa kusambaza vyandarua milioni 7.2 vyenye viatilifu vya muda mrefu katika kampeni maalumu kwa awamu kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Hadi sasa, watoto 117,000, sawa na asilimia 84 wenye umri chini ya miaka mitano, wamepata vyandarua katika Wilaya ya Mpanda mwezi wa Oktoba 2008

Iliyozinduliwa na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Peter Kayanza Pinda, (Mb) na watoto 349,641, sawa na asilimia 90.4, walipata vyandarua katika mkoa wa Tanga wakati wa Kampeni ya Surua iliyofanyika mwezi Agosti 2008 iliyozinduliwa na Makamu wa Rais, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein.



Mpango wa Mfuko wa Dunia wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria ulipitisha kiasi cha Dola za Kimarekani 113,000,000 mwezi Desemba 2008 kwa ajili ya kuwezesha kila kaya kupata vyandarua viwili vyenye viatilifu kwa ajili ya kinga dhidi ya Malaria.

Mpango wa kunyunyizia viuatilifu vya aina ya ICON majumbani, ambapo asilimia 90 ya kaya zilinyunyiziwa viuatilifu, hapo Juni, 2007 na Januari 2008, umeweza kuzuia milipuko ya malaria katika mkoa wa Kagera, hususani wilaya za Muleba na Karagwe.

UKIMWI

Katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Machi 2009, kumekuwa na ongezeko la huduma katika maeneo mbalimbali za kupambana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI kama inavyoainishwa katika jedwali:

Aina ya Huduma	2005	Machi 2009	Ongezeko
Idadi ya vituo vinavyopima Virusi vya UKIMWI kwa hiari	515	1,643	1,127
Idadi ya watu waliopima virusi vya UKIMWI kwa hiari	2,000,000	6,836,450	4,837,450
Idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya tiba na matunzo	96	418	322

Aina ya Huduma	2005	Machi 2009	Ongezeko
Idadi ya wagonjwa wanaopata tiba na matunzo	100,000	377,155	277,155
Idadi ya wagonjwa wanopata dawa za kutibu UKIMWI	23,951	205,879	181,928
Idadi ya vituo vinavyotoa hudumaya kuzuia maambukizo ya UKIMWI kwa mama mjamzito kwenda kwa motto	544	2,474	1,930

Idadi ya wananchi waliopima kwa hiari virusi vya UKIMWI imeongezeka kutokana na Kampeni ya Kitaifa iliyozinduliwa na kuongozwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete hapo tarehe 14 Julai 2007. Aidha, asilimia 34 ya wanawake wajawazito wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI walipata dawa za kuzuia maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Viwango vya maambukizi ya virusi vya UKIMWI nchini vimeshuka kutoka wastani wa asilimia 7 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 4.8 mwaka 2008.

Wizara imeandaa Mpango Mkakati mpya wa Kisekta wa kudhibiti UKIMWI wa kipindi cha miaka mitano (2008-2012). Mpango huo unalenga kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu za kudhibiti na kutibu UKIMWI nchini. Aidha, Mkakati wa Kuzuia Maambukizi mapya ya VVU/ UKIMWI kwa wafanyakazi wa Sekta ya Afya, ulitayarishwa na kuzinduliwa mwaka 2007 na umeanza kutumika. Aidha, miongozo na nyenzo za kufundishia masuala ya UKIMWI sehemu za kazi, zimeandaliwa na zinatumika.

Kifua Kikuu na Ukoma

Matibabu ya Kifua Kikuu yameboreshwa kwa kupunguza idadi ya vidonge kutoka 12 hadi 3 kwa siku kwa kutumia dawa mseto (Fixed Dose Combination - FDC). Aidha, kipindi cha matibabu kimepungua kutoka miezi 8 hadi 6. Pia, vituo vya kutibu Kifua Kikuu na Ukoma vimeongezeka kama ifuatavyo:

Ngazi ya huduma	Mwaka 2005	Mwaka 2008
Hospitali	185	203
Vituo vya Afya	450	628
Zahanati	1,000	2,218
Jumla	1,635	3,049

Kati ya mwaka 2005 hadi mwaka 2008 vituo vyote vya huduma vilikuwa na dawa za Kifua Kikuu na Ukoma za kutosha. Huduma shirikishi za Kifua Kikuu na UKIMWI, zimefika katika Halmashauri zote 132, ikilinganishwa na Halmashauri 3 mwaka 2005. Hadi kufikia mwezi Septemba 2008, asilimia 81 ya wagonjwa wa Kifua Kikuu walikuwa wamepima damu ili kubaini hali ya maambukizo ya virusi vya UKIMWI na kupatiwa matibabu.

Kuhusu kutokomeza Ukoma Tanzania imefikia kiwango cha chini cha utambuzi wa mgonjwa 1 kati ya watu 10,000 kulingana na mwongozo wa Shirika la Afya Duniani. Hivyo, Ukoma siyo tatizo kubwa la afya ya jamii hapa Tanzania. Viwango hivi vilifikiwa mwaka 2007 na Tanzania imepata tuzo kutokana na mafanikio hayo.

Magonjwa Mapya na yanayojitokeza Upya (Emerging and Re-emerging Deseases)

Wizara inaendelea kuchukua tahadhari ya magonjwa mapya yanayojitokeza. Kwa mfano maganjwa ya “Ebola”, “Marbug” ambayo yamejitokeza katika nchi jirani za Jamhuri ya Demokrasia ya Congo na Uganda. Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kwa ujumla pamoja na walioko karibu na nchi husika kuchukua tahadahri pamoja na kutoa taarifa haraka wanapoona mgonjwa mwenye dalili za magonjwa hayo. Aidha miongoni mwa magonjwa mengine yanaweza kujitokeza upya ni yale ambayo tunayadhibiti kwa njia ya chanjo ambayo ni kifaduro (Pertussis) na donda koo (Diphtheria). Ugonjwa mwingine ni wa Homa ya Bonde la Ufa ambao tunao uzoefu wa kukabiliana nao baada ya kujitokeza kwa mwaka 2007. Jumla ya wagonjwa wa Homa ya bonde la Ufa walikuwa 309 na vifo 138. Mikoa iliyoathirika ni Dodoma, Morogoro, Singida, Arusha, Manyara, Iringa, Pwani, Mwanza na Tanga. Hatua zilizochukuliwa kudhibiti ugonjwa ni: kuelimisha wananchi jinsi ya kujikinga na kuwahimiza kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa njia ya vipeperushi, matangazo, radio, televisheni, n.k; kutoa tiba kwa wale walipata ugonjwa; kuimarisha ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za ugonwa kwa ngazi mbalimbali pamoja na uwajibikaji; pia tulimarisha ushirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ambayo ilichanja mifugo.

Magonjwa yaliyopewa Kipaumbele (Neglected Tropical Deseases).

Wizara imeendelea kukabiliana na kudhibiti magonjwa ambayo yalisahaulika kwa kuwa na programu maalumu za kudhibiti magonjwa hayo ambayo ni ugonjwa wa matende na mabusha (Lymphatic filariasis), ugonjwa wa usubi (Onchocercasis), ugonjwa wa kichocho (Schistosomiasis), ugonjwa wa vikope (Trachoma), magonjwa ya minyoo yanayoambukizwa kwa njia ya udongo (Soil-transmitted helminths), ugonjwa wa malale (Human african trypanosomiasis), ugonjwa wa homa za vipindi (Relapsing fever) , n.k. Mkakati wa kudhibiti magonjwa haya kwa pamoja umeandaliwa (National Strategic Plan on NTDs). Halikadhalika serikali ya Marekani kupitia shirika lake la USAID wameahidi kusaidia fedha dola za kimarekani 700,000 kusaidia kutekeleza mpango huo. Katika kabiliana na ugonjwa wa matende na ngirimaji Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete alizindua Mfuko wa Rais wa kusaidia utoaji wa huduma za upasuaji wa ngirimaji.

Magonjwa yanayosambaa kwa wingi na kasi duniani (Pandermic)

Magonjwa yanayosambaa kwa wingi na kasi duniani ni pamoja na mafua makali ya ndege, virusi vya UKIMWI ambayo mikakati ya Kitaifa na Kimataifa inatumika kuyadhibiti magonwa hayo. Kwa upande wa Mafua Makali ya Ndege, wizara ina programu maalumu kwa kwa msaada wa CDC na imefungua vituo vitano (5) kwa ajili ya ufuatiliaji wa karibu wa kutambua virusi vinavyweza kusababisha mafua makali ya ndege katika hospitali ya wilaya ya Kibondo (Kigoma), hospitali ya Mwananyamala (Dar Es Salaam), hospitali ya Sekou Toure (Mwanza), hospitali ya Hydom (Manyara) na hospitali ya Dodoma. Kazi ya vituo hivi ni kutambua wagonjwa wenye dalili zinafanana na zile za mafua makali ya ndege na kuchukua sampuli na kupelekwa kwenye maabara ya kitaifa (National Influenza Centre) kwa ajili ya uchunguzi wa virusi vya ugonjwa huo. Maabara hiyo tayari ina uwezo wa kutambua virusi hivyo vya mafua makali ya ndege (Avian Influenza) pamoja na virusi vya Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley Fever).

Magonjwa yasiyo ya kuambukiza

Tatizo la magonjwa yasiyo ya kuambukiza limekuwa likiongezeka na kusababisha vifo vya watu hata katika umri mdogo (premature deaths). Magonjwa hayo ni Magonjwa ya moyo na kiarusi (Heart disease & Stroke), saratani, pumu, kisukari, ajali, akili na matumizi ya madawa ya kulevya, lishe duni, “sickle cell disease”, n.k.

Vidokezo vya hatari vinavyojitokeza na kuongezeka katika jamii yetu na ambavyo vinapelekea kupata magonjwa haya sugu ni pamoja na utumiaji wa tumbaku/uvutaji wa sigara, kunenepa sana, unywaji wa pombe wa kukithiri, kupanda kwa msukumo wa damu, kupanda kwa sukari katika damu mwilini, kupanda kwa mafuta katika damu mwilini, n.k. Kwa mfano katika utafiti ulifanyaika katika wilaya tatu nchini, takriban asilimia 12 ya watu wanavuta sigara, asilimia 29 hadi 71 wanakunywa pombe, asiliamia 11 hadi 16 ni wanene (obese), asilimia 19 hadi 36 msukumo wa damu uko juu na asilimia 12 hadi 16 mafuta katika damu yako juu.

Wizara inaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya maisha na tabia bora ili kukabiliana na magonjwa hayo yasiyo ya kuambukiza. Aidha Wizara imeandaa makakati maalumu kudhibit magonjwa yasiyo ya kuambukliza ambao utekelezaji wake hatimaye utapunguza tatizo la magonjwa hayo

Magonjwa yanayoenezwa na wadudu wadhurifu

Ufuatiliaji (Surveillance) wa viashiria na udhibiti wa ugonjwa wa homa ya malale uliofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Tabora umewezesha kudhibiti ugonjwa huo katika Halmashauri hiyo. Aidha, mlipuko wa ugonjwa wa tauni katika wilaya ya Lushoto umedhibitiwa katika kipindi cha miaka 3, kuanzia mwaka 2005 hadi 2008.

Afya ya Uzazi na Mtoto

Uzazi Salama

Huduma kwa wanawake wajawazito, kujifungua, chanjo, matibabu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na huduma za uzazi wa mpango zimeendelea kutolewa kwa gharama za serikali katika vituo vyote vya serikali vya kutolea huduma za afya nchini.

Mpango mkakati wa miaka saba (2008-2015) wa kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto umeandaliwa na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu wa Norway Mhe. Steltenberg, mwezi Aprili 2008. Mpango huu unatekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, na unalenga kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Miongozo mbalimbali imeandaliwa ili kuboresha utoaji huduma. Miongozo hiyo ni ya kutathmini vifo vya wanawake wajawazito, mtoa huduma uzazi salama, kumhudumia mama wakati wa kujifungua ili kuepuka kupoteza damu nyingi pamoja na mtaala wa mafunzo ya stadi za kazi kuhusu uzazi salama.

Mafunzo mbalimbali kwa watoa huduma ya afya kuhusu uzazi salama yametolewa mikoa yote Tanzania Bara. Jumla ya watoa huduma 2,379 wamepata mafunzo hayo. Aidha, watoa huduma 330 wamepata mafunzo ya jinsi ya kumhudumia mwanamke anapopata tatizo la kuharibu mimba.

Wizara kwa kushikiana na wadau imenunua magari 6 kwa ajili ya kubebea wagonjwa katika wilaya za Mafia, Kibaha, Ruangwa, Tukuyu, Mpanda na Nkasi. Ushirikiano wa wadau umeimarika hasa katika ngazi ya Taifa kwa kuwepo kwa mfumo wa kukutana, kupanga, kubadilishana uzoefu na utaalam wa utekelezaji wa masuala ya afya na maendeleo ya vijana.

Kumekuwa na ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vinatoa huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana kutoka asilimia 5 mwaka 2005 hadi asilimia 30 mwaka 2008.

Uzazi wa Mpango

Serikali kwa kushirikiana na wadau imenunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango kwa wakati katika wilaya zote na kwa kipindi chote hakukuwa na uhaba wa dawa hizi hapa nchini.

Mitaala ya kufundishia waalimu wa Uzazi wa Mpango (TOT), kitita cha mtoa huduma cha Uzazi wa Mpango na miongozo ya kwa ajili ya watoa huduma katika jamii (CBD) imepitiwa upya na kuboreshwa.

Mpango wa Taifa wa Chanjo
Viwango vya chanjo zote vimebaki kuwa zaidi ya asilimia 80% na kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano.

Wizara imeendesha kampeni ya kutokomeza ugonjwa wa Surua nchini kwa watoto wenye umri kati ya miezi 9 hadi miaka 10. Jumla ya watoto 10, 567,104 walichanjwa. Aidha, chanjo ya polio ilitolewa katika wilaya 18 za mipakani na zenye viashiria vya kuambukiza polio. Jumla ya watoto 1,459,162 walipata chanjo ya polio. Viwango vya chanjo ya polio vimefikia zaidi ya asilimia 90 na mgonjwa wa mwisho wa polio hapa nchini alipatikana Julai mwaka 1996.



Pikipiki 121 zimenunuliwa na kusambazwa katika halmashauri ili kuboresha huduma za chanjo na afya kwa jumla. Aidha, jumla ya majokofu 1,722 yanayotumia nishati ya gesi na mionzi ya jua yamesambazwa katika maeneo yasiyo na nishati ya umeme kwa ajili ya kuhifadhia chanjo.

Udhibiti wa Magonjwa ya Watoto kwa Uwiano
Wizara imewezesha halmashauri zote kutekeleza mpango wa udhibiti wa magonjwa ya Watoto kwa Uwiano (Integrated Management of Child Illness - IMCI) ili kuboresha matibabu kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Vitabu, miongozo ya mafunzo na vielelezo mbalimbali vilichapishwa na kusambazwa katika wilaya. Miongozo na vitabu hivyo ni pamoja na Mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya utunzaji wa watoto wachanga wenye uzito pungufu (Kangaroo Mother Care Guidelines), Mwongozo wa Mafunzo kwa ajili ya Utunzaji wa Watoto Wachanga (Essential Newborn Care). Aidha, nakala 6,000 za miongozo ya kufundishia (training modules), nakala 8,000 za vitabu vya mazoezi (exercise modules), nakala 1,000 za mwongozo wa IMCI pamoja na vijarida vilichapishwa na kusambazwa nchini. Pia vipeperushi vinavyoonesha mabadiliko mapya ya matibabu ya mtoto vimeandaliwa na kusambazwa.

Kupungua kwa vifo vya watoto

Utekelezaji wa afua mbalimbali umechangia kwa kiwango kikubwa kupunguza vifo vya watoto. Mafanikio haya yanaashiria kuwa kuna uwezekanao mkubwa wa kufikia lengo la nne la Maendeleo ya Milenia (MDG 4)



WW – Watoto wachanga, SA- Siku 40 za uzazi, VWW- Vifo vya watoto wachanga, VW – Vifo vya watoto, V5W- Vifo vya watoto chini ya miaka 5.

Huduma ya Udhibiti wa Saratani

Vituo 33 vya kupimia wanawake saratani ya matiti na shingo ya kizazi vimeanzishwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Dodoma, Lindi, Pwani, Tanga, Mwanza, morogoro, Ruvuma, Kilimanjaro na Iringa.

Kwa kushirikiana na Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), wanawake zaidi ya 63,895 wamechunguzwa kutambua dalili za saratani ya matiti kupitia kampeni zilizofanyika mikoa 7 ya Dar es Salaam Mbeya, Mwanza, Lindi, Mtwara, Manyara na Dodoma. Kupitia kampeni hizo, asilimia 4 ya wanawake 2978 waliopatikana na matatizo ya matiti, walikuwa na saratani na walipatiwa matibabu katika vituo vya tiba vya Serikali. Aidha, kwa kushirikiana na wadau kutoka Marekani, mashine 5 za kuchunguza matiti “Mammograph machine” zilipatikana na kuwekwa katika hospitali za Lindi, Kibaha, Amana, Ocean Road na Arusha.

Huduma ya Afya ya Msingi katika Jamii
Usimamizi na ufuatiliaji wa huduma zinazotolewa katika ngazi ya jamii umefanyika katika Mikoa 14 na Halmashauri 38 katika Mikoa ya Mbeya, Lindi, Tabora, Manyara, Mwanza, Morogoro, Kagera, Iringa, Dodoma, kilimanjaro, Tanga, Mtwara na Pwani. Halmashauri za Kyela, Rungwe, Mbozi. Ruangwa, Nachingwea, Lindi. Urambo, Sikonge, Uyui. Mbulu, Babati, Karatu, Sengerema, Geita, Kwimba, Kilosa Morogoro, Mvomero, Bukoba, Muleba. Njombe, Ludewa, Makete, Kongwa, Kondoa, Chamwino. Hai, Mwanga, Halmashauri ya wilaya ya Moshi. Manispaa ya Tanga, Muheza, Mkinga. Mtwara, Tandahimba Newala. Rufiji, Kisarawe, Mkuranga, Lushoto, Muheza na Korogwe.

Huduma ya Macho
Wizara kwa kushirikiana na wadau wa huduma za macho imeandaa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Huduma za Macho wa miaka mitano (2009 – 2013). Aidha, kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mpango Kabambe wa miaka mitano, (2008-2012) wa kudhibiti ugonjwa wa Vikope [Trachoma], katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

Utafiti wa ugonjwa wa usubi umefanyika katika Halmashauri za Wilaya za Mufindi na Njombe na kugundulika kuwa na kiwango kikubwa cha ugonjwa wa usubi. Aidha, tathimini ya kuangalia uendelevu wa Miradi ya Usubi katika mikoa ya Morogoro na Ruvuma ilifanyika kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO), ambapo halmashauri zimeanza kuingiza shughuli za kudhibiti Usubi katika Mipango Kabambe ya Wilaya (CCHP).

Mpango Mkakati wa kutokomeza Usubi wa miaka mitano wenye lengo la kutokomeza ugonjwa wa usubi hapa nchini umekamilika., umeandaliwa na uko katika hatua za mwisho za kukamilishwa.

Huduma za Afya Shuleni
Wizara iliendesha Kampeni na kugawa dawa za kichocho (Praziquantel) na minyoo (Albendazole/Mebendazole) kwa wanafunzi wa shule za msingi. Wanafunzi walengwa waliopata dawa 2005 ni asilimia 78 na 2007 ni asilimia 85.

Huduma za Elimu ya Afya kwa Umma
Wizara inaendelea kuelimisha wananchi njia za kujikinga na kudhibiti maradhi kupitia vipindi vya redio, magazeti na televisheni. Jumla ya vipindi vya redio 208 vya “Siri ya Afya Bora” vilirushwa hewani. Mada zilizotolewa ni pamoja na umuhimu wa maji na usafi wa mazingira, makazi na vyoo bora, mazoezi ya viungo, lishe bora, afya shuleni, uzazi salama, unyonyeshaji bora, umuhimu wa chanjo, matumizi sahihi ya dawa, damu salama.na tiba asili.

Aidha, mada nyingine zilikuwa juu ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma, Malaria, Kipindupindu, Magonjwa ya kuharisha, homa ya matumbo, magonjwa ya utotoni, magonjwa ya macho na upofu, Kichaa cha mbwa, Kifafa, Kisukari,

madhara ya tumbaku, Saratani, Homa ya uti wa mgongo, Homa ya Bonde la Ufa, Ebola na Homa ya Mafua ya ndege.

Vielelezo mbalimbali vilisambazwa vikiwemo vipeperushi na mabango ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kujikinga na maradhi yakiwemo homa ya bonde la ufa, mafua ya ndege, kichaa cha mbwa, kipindupindu, homa ya matumbo, kisukari, umuhimu wa mazoezi ya viungo kwa afya na madhara ya tumbaku.

Wizara ilianzisha mtandao wa waandishi wa habari wa masuala ya afya, (Tanzania Health Writers' Network) ili kutoa taarifa sahihi kuhusu afya ya jamii.

Huduma za Tiba

Huduma za tiba zinatolewa kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Serikali. Huduma zinazotolewa ni pamoja na tiba, uchunguzi, dawa na vifaa pamoja na kurufaa wagonjwa ngazi moja hadi nyingine. Huduma zilitolewa kwa vituo vifuatavyo

Ngazi	2006	Machi 2009
Zahanati	3,280	3,649
Vituo vya Afya	347	395
Hospitali za Wilaya na Teule	86	90
Hospitali za Taasisi	3	6
Hospitali za Rufaa –Mkoa	18	18
Hospitali Maalum	5	5
Hospitali za Kanda	3	3
Hospitali ya Taifa	1	1

Afya ya Kinywa

Vituo 270 vya kutolea huduma ya dharura ya tiba ya meno (Emergency Oral Health Care) vimeanzishwa nchi nzima. Tabibu 270 wa vituo hivyo wamepewa mafunzo maalum ya jinsi ya kutoa huduma za kinywa pamoja na kupewa vifaa. Aidha, halmashauri 91 zilipewa vifaa vya tiba ya meno (Dental Equipment).

Mashirika ya Kujitolea na Binafsi (Voluntary and Private Organizations)

Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu huduma za afya zinazotolewa na mashirika ya kujitolea, na watu binafsi katika vituo kama ifuatavyo.

Ngazi	2006	Machi 2009
Zahanati	1,704	1,873
Vituo vya Afya	153	182
Hospitali za Teule za Wilaya	21	25
Hospitali za Kawaida (VA)	92	96
Hospitali za Rufaa-Mkoa	18	21
Hospitali Maalum	1	1
Hospitali za Kanda	2	2

Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitayarisha mkataba maalumu wa utoaji huduma kati ya halmashauri na vituo vya matibabu binafsi (Service Agreement) kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

Wizara imeongeza ruzuku kwa mashirika ya kujitolea/dini kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 50,000 kwa kitanda kwa mashirika ambayo yanatoa huduma katika maeneo ambayo serikali haina vituo vya kutolea huduma.

Huduma za Maabara na Ufundi wa Vifaa Tiba

Maabara za Wilaya, Mikoa na Rufaa zimepewa mashine za kuchunguza damu na uwezo wa figo na ini pamoja na chembe chembe za kinga – CD4 kwa ajili ya uanzishwaji na ufuatiliaji wa matibabu ya wagonjwa wa UKIMWI.

Maabara zote za Kanda zimepewa mashine maalum (DNA PCR) kwa ajili ya kuchunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU) kwa watoto wachanga chini ya miezi 18.

Maabara zote za Kanda ziko kwenye mchakato wa kurasimishwa katika Ithibati ya viwango vya Kimataifa vya Ubora wa Huduma za Maaabara (Laboratory Accreditation On International Standards). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Centre for Desease Control (CDC) ya Marekani imejenga Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii katika eneo la NIMR/CDC. Maabara hiyo, itahusika na uchunguzi wa magonjwa ya milipuko ikiwemo homa ya bonde la ufa pamoja na kusimamia na kutoa mafunzo ya uhakiki wa ubora wa Huduma za maabara (Laboratory Quality Assurance).

Wizara imebadilisha utaratibu wa kitaifa wa upimaji wa haraka wa VVU (National HIV rapid testing algorithm) kwa kutumia 'Capillus' iliyohitaji kutunzwa kwenye ubaridi na kutumia 'SD Bioline isiyohitaji kutunzwa kwenye ubaridi.

Maabara za Hospitali za Rufaa 2, Mikoa 2 zimepewa jumla ya Kompyuta 37. Hospitali hizo ni Bugando kompyuta 14, Hospitali ya Rufaa Mbeya 11, Shinyanga 5, Ruvuma 5 na Wizara 2 kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa taarifa za Maabara kwa njia ya kompyuta (Electronic Laboratory Information System).

Vyuo vya maabara ngazi ya cheti (Laboratory Assistants) vimeongezeka kutoka 3 hadi 5. Aidha, mafunzo ya Shahada kwa Wataalamu wa Maabara yameanzishwa katika Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili. Pia, mtaala wa vyuo vya Maabara vya ngazi ya Stashahada (Diploma in Medical Laboratory Sciences) umepitiwa na kurekebishwa ili kuingiza elimu ya upimaji wa maambukizi ya VVU, uhakiki wa ubora wa vipimo vya maabara na Menejimenti ya huduma za maabara.

Mafunzo ya kujiendeleza na ya muda mfupi kwa wataalamu wa maabara kuhusu uchunguzi wa magonjwa na utumiaji wa vifaa vya kisasa vya Maabara yametolewa katika mikoa na wilaya zote. Aidha, mchakato wa mafunzo ya Stashahada ya ufundi wa vifaa tiba umeanzishwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Ufundi ya Dar es Salaam. Udahili wa wanachuo wa ufundi wa vifaa tiba utafanyika Septemba, 2009.

Huduma za Radiolijia

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imepata "Magnetic Resonance Imaging" (MRI) na mashine nne za Ultra Sound. Wilaya tatu za Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na wilaya za Chato (Kagera), Tandahimba (Mtwara) Bukombe (Shinyanga) zimenunuliwa X-Ray mashine kwa ushirikiano na Serikali ya Uholanzi kupitia mradi wa "Overseas Related Export Trade – ORET".

Wizara imeanzisha mpango wa kitaifa wa upatikanaji wa Damu Salama nchi nzima. Hivi sasa kuna vituo sita vya Kanda vinavyofanya kazi. Vituo hivyo vipo Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kaskazini (Kilimanjaro), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Mashariki Makao Makuu (Dar es Salaam), Kanda ya Magharibi, Tabora na Kanda ya Kusini, Mtwara.

Karakana tano (KCMC, BMC, MNH, MRH na Ligula Mtwara) za kanda za matengenezo ya vifaa tiba zimeboreshwa kwa kupewa nyenzo na magari na pia mafundi wamepewa mafunzo maalumu. Vifaa tiba vya hospitali katika kanda hizo hivi sasa vinafanyiwa matengenezo ya kinga.

Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba

Zahanati na vituo vya afya vya Serikali 4,045 vinapewa dawa na vifaa tiba. Aidha, Wizara kupitia Bohari ya Dawa imeanzisha mfumo wa Integrated system (ILS)" wa uagizaji wa dawa kulingana na mahitaji na mgao wa fedha.

Mwongozo wa Tiba na Orodha ya Dawa Muhimu (Standard Treatment Guideline + Essential Drugs List) umeandaliwa ili kuboresha utoaji sahihi wa dawa.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2006/07, 2007/08 na 2008/09 kumekuwa na ongezeko la bajeti ya dawa na vifaa mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo



Afya ya Akili na Madawa ya Kulevya
Wizara imekamilisha na kusambaza mkakati wa Taifa wa huduma ya afya ya akili 2006. Aidha, Sheria ya Afya ya akili ya mwaka 2008, imepitishwa na Bunge.

Wizara imeanzisha huduma ya afya ya akili ngazi ya msingi katika mikoa ya Morogoro, Mtwara, Mwanza, Shinyanga na Tanga. Jumla ya Madaktari 22 wamepewa mafunzo ya muda mfupi wa kutibu wagojwa wa akili katika hospitali za mikoa na wilaya.

Ujenzi wa kituo maalum cha matibabu na utengemao (Rehabilitation services) wa waathirika wa pombe na vilevi vingine, unaendelea katika hospitali ya Mirembe, Dodoma.

Magonjwa yasiyoambukizwa
Wizara imeandaa Mkakati wa Taifa wa Huduma ya magonjwa yasiyombukiza mwaka 2008. Mkakati huo tayari umesambazwa kwa Waganga Wakuu wa Wilaya na Mikoa kwa ajili ya kutumika nchini.

Tiba Asili na Tiba Mbadala
Wizara inaadhimisha siku ya Tiba Asili ya Mwafrika (African Traditonal Medicine Day) kila mwaka kuanzia mwaka 2004. Aidha, Wizara imeandaa Mwongozo wa kufundishia Waganga wa Tiba Asili.

Rufaa na Wagonjwa wa Nje
Mwaka 2008, Wizara ilipeleka wagonjwa 741 kutibiwa nje ya nchi. Aidha, Wizara imeongeza fedha za matibu ya wagonjwa nje ya nchi kutoka bilioni 1.9 mwaka 2007/08 hadi kufikia shilingi bilioni 4 kwa mwaka 2008/09.

Huduma ya Upasuaji wa moyo imeanzishwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Aidha, upasuaji na uwekaji viungo bandia vya nyonga na goti (hip and knee replacement) unafanyika katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) ili kupunguza gharama ya kepeleka wagonjwa nje ya nchi.

Mafunzo

Wizara inapanga na kusimamia mafunzo ya afya katika vyuo 74 vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha, inaratibu ubora wa mafunzo yatolewayo na vyuo 42 vinavyomilikiwa na mashirika ya dini na binafsi. Pia, Wizara inasimamia mafunzo ya kujiendeleza ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa sekta ya afya.

Mipango ya Watumishi wa Afya

Wizara imeandaa na kukamilisha Mpango Mkakati wa Watumishi wa Sekta ya Afya 2008- 2013, unaotoa dira na kuweka malengo ya kuboresha maendeleo na matumizi ya rasilimali watu katika sekta ya afya.

Wizara imekamilisha maandalizi ya kujumuisha taarifa za watumishi wa afya katika Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya nchini (MTUHA). Mfumo huo utarahisisha upatikanaji wa taarifa za rasilimali watu katika ngazi mbalimbali za utoaji huduma za afya.

Elimu Endelevu

Wizara imeandaa na kukamilisha moduli za mafunzo ya uendeshaji kwa viongozi ngazi ya ngazi ya zahanati na kituo cha afya. Aidha, mafunzo ya uendeshaji tayari yametolewa katika ngazi ya halimashauri na mkoa. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau imefanya tathimini ya mafunzo ya kujiendeleza kwa njia ya masafa marefu. Vilevile, Mipango mikakati kwa kanda nane za mafunzo imekamilika na kuzinduliwa rasmi mwezi Februari 2009**.**

Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanzisha mafunzo ya stashahada ya uongozi kwa njia ya masafa. Wanafunzi wapatao 91 wanatarajiwa kuhitimu mafunzo hayo mnamo Juni 2009. Aidha, idadi ya wanafunzi wa mafunzo ya uzamili imeongezeka kila mwaka. Mwaka 2005/06, wanafunzi 61 walidahiliwa, mwaka 2006/07 wanafunzi 130, mwaka 2007/08 wanafunzi 148 na mwaka 2008/09 wanafunzi 170.

Orodha ya vitabu muhimu kwa ajili ya vyuo vya afya imeandaliwa na imekamilika kulingana na mahitaji (essential book list for the health training institution was developed according to the requirements).

Sayansi Shiriki na Uuguzi (Allied Health and Nursing)

Wizara imeongeza wahitimu wa mafuzo mbalimbali kutoka 2,858 mwaka 2005 hadi kufikia 3,038 mwaka 2008 katika kada za Madaktari Wasaidizi,Tabibu, Maafisa Afya, Mafundi Sanifu Maabara, Dawa, Macho na Wauguzi.

Wizara imeongeza wanafunzi watarajali (Pre-Service) katika vyuo vya afya kutoka 1,013 mwaka 2005 hadi kufikia 3,831 mwaka 2008. Ongezeko hili la asilimia 278 litawezesha Serikali kupata mafanikio katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM).

Udahili wa Wanafunzi

MWAKA	2005/06	2006/07	2007/08	2008/09
Idadi ya wanafunzi Watarajali waliodahiliwa Sayansi Shiriki	493	497	575	1,520
Idadi ya wanafunzi Watarajali waliodahiliwa Uuguzi	520	611	745	2,311
JUMLA	**1,013**	**1,108**	**1,320**	**3,831**

Wizara imepitia na kukamilisha mitaala 6 na kupunguza muda wa mafunzo darasani kwa mwaka mmoja kwa baadhi ya kada. Mitaala hiyo ni ya Wazoeza Viungo, Tabibu, Tabibu Wasaidizi, Mafundi Sanifu Macho na Wauguzi.

Wizara imerejesha mafunzo ya kada ya Tabibu Msaidizi na Muuguzi Mkunga Daraja la "B" kwa ajili ya zahanati. Mafunzo ya kada hizo yatakuwa ya miaka miwili badala ya miaka mitatu.

Vyuo vya afya vipatavyo 93 vimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (National Accreditation Council for Technical Education - NACTE). Vituo 45 vipo katika hatua mbalimbali za kupata ithibati.

Ustawi wa Jamii

Huduma ya Watu wenye Ulemavu na Wazee

Muswada wa Sheria Jumuishi ya Watu wenye Ulemavu na Wasiojiweza "Disability Bill" umeandaliwa ili kubadili sheria Namba 2 ya ajira na Sheria Namba 3 ya Matunzo kwa Watu Wenye Ulemavu na Wasiojiweza. Aidha, Mkataba wa Kimataifa juu ya haki ya watu wenye ulemavu umeandaliwa.

Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, inakusanya takwimu ili kubaini mahitaji ya watu wenye ulemavu. Aidha, Wizara imeunda na kuzindua Kamati ya Kitaifa ya Muongo wa Watu Wenye Ulemavu.

Wizara imegharamia timu ya wadau 7 wakiwemo Askari, Waandishi, Maafisa Ustawi wa jamii na Viongozi wa Chama cha Maalbino kwenda katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa lengo kutambua chanzo na ukubwa wa tatizo la vitendo vya ukatili na mauaji ya maalbino.

Ustawi wa Familia
Jumla ya familia 2,250 zilipata huduma ya ushauri nasaha na usuluhishi wa ndoa zenye migogoro. Aidha, familia 450 zisizokuwa na uwezo na kuathiriwa na UKIMWI zilipata msaada wa dharura.

Ustawi na Maendeleo ya Mtoto
Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imeandaa Mpango wa Kazi 2007 – 2010 wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi (National Costed Plan of Action 2007 – 2010) ambao unatekelezwa na wadau mbalimbali. Nakala 5,000 za mpango huo zimesambazwa.

Wizara imeandaa mwongozo wa uwezeshaji haki jamii kuwasaidia watoto walio katika mazingira hatarishi kupata haki za kisheria. Wawezeshaji 25,000 wamepewa mafunzo ya uwezeshaji haki jamii katika halmashauri 26, lengo ni kizifikia halmashauri zote nchini.

Mpango wa utambuzi wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi unatekelezwa katika halmashauri 78. Jumla ya watoto 511,820 wametambuliwa kuwa katika mazingira hatarishi. Kati ya hao wasichana ni 245,674 na wavulana ni 266,146. Aidha, watoto wapatao 432,322 wamepewa huduma mbalimbali ambazo ni pamoja na vifaa vya shule, karo, kujengewa/kukarabatiwa nyumba zao au za walezi wao, msaada wa chakula, huduma za afya na ushauri wa kisaikolojia na kisheria.

Maafisa Ustawi wa Jamii na watoa huduma 173 katika halmashauri 53 wamepewa mafunzo ya kukusanya, kutunza na kutumia takwimu za watoto walio katika mazingira hatarishi.

Usimamizi wa Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi
Wizara imeandaa mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa makao ya watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi. Hadi kufikia Desemba, 2008 yapo makao 83 yanayohudumia watoto 3,238. Aidha,Wizara imeandaa mwongozo wa malezi ya kambo na kuasili. Hadi kufikia mwaka 2008 Wizara ilipokea maombi ya malezi ya kambo 168 kati ya hayo 54 yamepata kibali.Watoto 36 wameasiliwa.

Maelezo	**2006**	**2007**	**2008**
Maombi yaliyopokelewa	42	45	44
Maombi yaliyopata vibali	15	12	16
Watoto walioasiliwa mahakama kuu	12	7	9

Malezi ya Awali
Mtaala wa mafunzo ya malezi ya watoto wadogo umepitiwa na kuingiza masuala mapya yanayohusu malezi kwa watoto wanaoishi na VVU na utambuzi wa awali kwa watoto wenye ulemavu. Aidha, Wizara imeandaa

mwongozo wa uwezeshaji wa malezi changamshi ya awali kwa watoto wadogo pamoja na makala mbalimbali za kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa malezi kwa watoto wadogo.

Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto,Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mtandao wa Malezi Tanzania inatekeleza mpango jumuishi wa kutoa huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali kwa watoto wadogo (Intergrated Early Child Development (ECD) Service Delivery). Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana 51 vimesajiliwa kati ya 180 vilivyowasilisha maombi, na kufanya idadi kufikia vituo 442. Mafunzo ya malezi ya watoto wadogo yametolewa katika vyuo 12, ambapo walezi 996 walipata mafunzo hayo.

Huduma za Marekebisho ya Tabia kwa Watoto na Vijana
Wizara imefanya ukarabati wa majengo ya mahabusi 5 za mkoa wa Arusha, Moshi, Tanga, Mbeya na Dar Es Salam na Shule ya Maadilisho 1 ya Mkoa wa Mbeya. Aidha, Wizara imeandaa kitabu cha maadili ya Maafisa Haki za Mtoto na Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Code of Conduct na Customer Care Service).

Taasisi ya Ustawi wa Jamii
Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeanzisha mafunzo ya Shahada (National Technical Award - NTA Level 8) katika fani za Huduma ya Ustawi wa Jamii, Rasilimali Watu na Mahusiano kazini. Aidha, imeanzisha Stashahada za Kawaida (NTA Level 6) na mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Sheria , Usuluhishi na Uamuzi.

Udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka 1,036 mwaka wa masomo 2005/06 hadi kufikia 2,496 mwaka wa masomo 2008/09 ambayo ni sawa na asilimia 141. Katika mwaka wa masomo 2008/09 idadi ya wanafunzi wa kiume ni 1,086 na wanawake ni 1,410 ambao ni asilimia 56 ya wanafunzi wote.

Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeanzisha mafunzo ya “Para Social Workers” kwa ajili ya kuwahudumia watoto yatima wanaotokana na tatizo la UKIMWI. Mafunzo yanaendeshwa na Taasisi ya Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Jane Addams School of Social Work- kutoka Chuo Kikuu cha Chicago, Illinois nchini Marekani kwa uhisani wa American International Health Alliance.

Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeajiri walimu wapatao 15 kutokana na ongezeko la wanafunzi. Aidha, Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii inaendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa na unatarajiwa kukamilika mwaka 2009/10 na utagharimu shilingi bilioni 3.6.

Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii imepata eneo la ekari 165 katika Kijiji cha Msoga Wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya upanuzi wa Taasisi.

Fedha na Uhasibu

Matumizi ya Fedha

Wizara imeandaa taratibu za matumizi ya fedha kwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali. Sheria hizo ni pamoja na manunuzi, usimamizi wa fedha za umma na kanuni zake. Aidha, sheria na miongozo zinafanyiwa mapitio mara kwa mara ili kukidhi mahitaji ya utekelezaji. Wizara inahakikisha kuwa fedha zinatumika katika maeneo yaliyopangwa na kukubalika. Pia ukaguzi wa mara kwa mara unafanyika katika maeneo hatarishi. (Risk Areas).

Kuhusu matibabu ya wagonjwa nje ya nchi, Wizara inatumia Balozi katika kusimamia malipo ya matibabu. Inapobidi Wizara hutuma Maafisa na Wakaguzi kukagua nyaraka kama kuna mashaka kabla ya kulipa ili kusuluhisha kabla malipo kufanyika. Malipo kwa ajili ya kazi nje ya Wizara kama vile mafunzo kwa watoa huduma na ufuatiliaji yanalipwa kupitia Hazina ndogo kwa ajili ya usalama wa fedha.

Katika kutekeleza mwongozo wa Hazina, Wizara imeanzisha Kamati ya Ukaguzi kwa ajili ya kufuatilia mapato na matumizi na utekelezaji wa mpango kazi wa Wizara. Aidha, Wizara imefanya maboresho katika maeneo mbalimbali ili kudhibiti matumizi ya fedha na mali ya umma. Pia, Wizara imeweka utaratibu wa kuandaa Mpango wa ununuzi na kuingiza vifungu vyote vya bajeti.

Utoaji wa taarifa za fedha na utekelezaji wa Bajeti

Wizara imeendelea kutoa taarifa hizi kwa wakati na hivyo kurahisisha ulinganishaji takwimu za miaka ya nyuma kwa kutumia mtandao wa malipo na Fedha zilizowekwa hazina (IFMS) kama inavyoainishwa kwenye jedwali

Malipo na Fedha zilizotolewa na Hazina

Matumizi ya kawaida	**Bajeti**	**Gawio**	**Matumizi**
2004-05	105.08	105.08	104.16
2005-06	171.59	152.81	150.87
2006-07	181.21	178.98	178.98
2007-08	192.88	174.05	173.22
Bajeti ya maendeleo	**Bajeti**	**Gawio**	**Matumizi**
2004-05	91.22	72.31	71.71
2005-06	103.44	84.25	84.23
2006-07	96.30	94.72	94.72
2007-08	181.94	118.18	108.77





Kwa Mwaka 2008 Wizara ilichukua ushindi wa kwanza kwa kutengeneza hesabu zake za mwaka zinazokidhi viwango vya kimataifa yaani International Public Sector Accounting Standard (IPSAS).

Ukusanyaji wa Mapato

Kumekuwa na ongezeko la mapato halisi yatokanayo na uchangiaji huduma kwa kipindi cha kuanzia Desemba 2005 hadi Desemba, 2008 kutoka shilingi bilioni 1.3 hadi kufikia shilingi bilioni 2.1, kutokana na ada za mafunzo, usajili wa maabara binafsi na vifaa vya maabara, uandikishaji wa hospitali binafsi na uchangiaji huduma za matibabu.

Kulipa Mishahara na malimbikizo

Kazi ya ulipaji mishahara na marupurupu ya watumishi imeendelea. Wizara imeweka utaratibu wa kufuatilia watumishi waliopo mikoani ili kubaini kuwepo kwa watumishi hao ili kusaidia kuhakiki taarifa zinazopokelewa, pamoja na kusikiliza matatizo yao kwa lengo la kuharakisha haki za madai ya mtumishi.

Utekelezaji wa Maagizo ya Wakaguzi na Kamati za Bunge
Wizara imetekeleza kikamilifu maagizo yote ya wakaguzi wa mahesabu ya fedha na Kamati za Bunge. Aidha, imepunguza hoja za Ukaguzi kwa zaidi ya asilimia 50% kutoka hoja 60 za Ukaguzi kwa mwaka 2004/2005 hadi kufikia hoja 23 kwa mwaka 2007/08. Pia,ukaguzi maalum wa mtandao wa bohari kuu ya dawa (MSD) ulifanyika ili kuthibitisha ubora wa mtandao huo.

Ukaguzi Wa Ndani
Wizara imeimarisha usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine kwa kuandaa mwongozo wa malipo.

Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), Mamlaka ya Kusimamia Manunuzi ya Umma (PPRA) pamoja na Chuo Kikuu Mzumbe imeendesha mafunzo kwa Wakuu wa Idara na watumishi wengine juu ya Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2001 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.
Wizara imeendesha mafunzo ya kutambua maeneo yenye vihatarishi vya kufikia malengo (risk areas). Mafunzo haya yameiwezesha wizara kuorodhesha maeneo hatarishi katika daftari (Risk Management Register) na kuweka mikakati ya namna ya kukabiliana nayo.

Wizara imeweka mifumo ya kuboresha udhibiti (Internal Control Systems) ambayo imeiwezesha kusimamia rasilimali za serikali na kupunguza hoja za ukaguzi kwa zaidi ya asilimia 50 kutoka hoja 60 kwa mwaka 2004/05 hadi kufikia hoja 23 kwa mwaka 2007/08.

Wizara imebadilisha mfumo wa kupeleka fedha za utekelezaji wa shughuli zinazofanyika mikoani. Taasisi za Wizara zilizopo mikoani zimepewa jukumu la kupokea na kusimamia fedha kwa kushirikiana na Hazina Ndogo au Wahazini wa halmashauri. Hatua hii imesaidia kupatikana kwa taarifa za matumizi ya fedha, kazi zilizofanyika na kumbukumbu za serikali na kurahisisha ukaguzi wa kazi zilizofanyika. Aidha, hatua hiyo imeongeza usalama wa fedha za serikali kwa kuwa hakuna mtumishi anayepewa na kutembea na fedha nyingi.

Wizara imeandaa Daftari la Kumbukumbu za vifaa/mali za serikali (Master Inventory Register) pamoja na Daftari la Vifaa vya Kudumu kwa Muda Mrefu. (Fixed Asset Register).

Ununuzi
Wizara imepeleka waraka wa kukasimu majukumu ya ununuzi (Delegation and Contract Out) kwa Bodi ya Zabuni ya Wizara na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Taasisi mbalimbali. Aidha, Wizara imeandaa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka ambao umewasilishwa na kuidhinishwa na Mamlaka ya Kusimamia Manunuzi ya Umma (PPRA) na wahisani wa Mfuko wa Pamoja (Basket Fund).

Ushauri wa kitaalam kuhusu masuala ya ununuzi umeimarishwa katika Taasisi na miradi mbalimbali inayogharamiwa na Serikali na Mfuko wa Pamoja (Basket Fund). Taasisi hizo ni pamoja na Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), TFDA, Ocean Road Hospital, KCMC, Bugando, MSD, na Halmashauri na Mikoa.

Daftari la vifaa vya kudumu (Fixed Asset Register) limeboreshwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeandaa mpango wa kuboresha Kitengo cha Ununuzi.

Mawasiliano
Kitengo cha mawasiliano ni kiungo kati ya Wizara na vyombo vya habari pamoja na wananchi katika kufafanua mambo mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara.

Kuwepo kwa Msemaji wa Wizara kumerahisisha upatikanaji wa habari kwa haraka kuliko ilivyokuwa awali ambapo taarifa zilikuwa zikitolewa na viongozi wa juu tu. Ufafanuzi na upatikanaji wa habari za Wizara kwa wananchi na wadau umerahisishwa.

Wizara imeanzisha utaratibu wa kuweka taarifa katika tovuti yake. Aidha, Wizara inafafanua mambo mengi kwa wananchi kupitia mikutano na vyombo vya habari.

Hospitali Maalum

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili
Hospitali ya Taifa Muhimbili hutoa huduma za kibingwa za tiba, mafunzo na utafiti.
Ukarabati wa majengo ya kutolea huduma za afya na kuweka vifaa na samani mpya vimekamilika. Ukarabati huo umetumia fedha za serikali na mkopo kutoka Benki ya Afrika (ADB). Katika kipindi cha mwaka 2005 – 2008. Ukarabati ulihusu Maabara Kuu (Central Pathology Laboratory –CPL), vyumba vya upasuaji, wodi, huduma za Radiolojia na jengo la kuhifadhia maiti. Aidha, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kwa ajili ya ushauri nasaha na matibabu na uzio kuzunguka Hospitali umekamilika.

Mashine ya MRI imenunuliwa na inatumika. Mashine hiyo imesaidia kupunguza idadi ya wagonjwa waliokuwa wakilazimika kwenda nje ya nchi kufuata kipimo hicho. Jumla ya wagonjwa 122 wamepimwa tangu mashine ianze kufanya kazi tarehe 14 Desemba 2008. Aidha, huduma za upasuaji wa moyo zinafanyika MOI. Wagonjwa 71 wamefanyiwa upasuaji wa moyo tangu April 2008.

Huduma za kumbukumbu za hospitali zimeboreshwa kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Mfumo huo unawezesha utunzaji na ufuatiliaji wa taarifa za wagonjwa, makusanyo ya mapato, huduma za maabara na ununuzi wa dawa na vifaa.

Tiba ya macho inatolewa kwa kutumia kifaa kiitwacho “laser” ambacho huwezesha kutoa tiba ya macho bila upasuaji wa kawaida.

Hospitali ya Rufaa ya Bugando

Hospitali ya Rufaa ya Bugando inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, inahudumia wakazi wa mikoa 6 ya Kanda ya Ziwa yaani Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Tabora na Shinyanga. Mikoa hiyo inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi milioni 13. Hospitali ina jumla ya vitanda 850.

Hospitali hiyo inazalisha dawa za sindano za “infusions” za aina mbalimbali za kutosheleza asilimia kubwa ya mahitaji yake. Chupa za dawa hizo zipatazo 56,000 zinazalishwa kwa mwaka.

Hospitali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Mt. Augustine inafundisha madaktari. Mwaka 2008, madaktari 13 walihitimu kwa mara ya kwanza. Aidha, hospitali hiyo inatoa mafunzo ya Madaktari Wasaidizi, Radiolojia, Uuguzi, Dawa na Maabara.

Hospitali imekamilisha chumba cha kisasa kwa ajili ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu (Intensive Care Unit - ICU). Aidha, imepanua chumba cha kuhifadhia maiti kutoka majokofu ya kuhifadhia maiti 20 hadi 53. Pia, imekamilisha ukarabati wa mabweni ya wanachuo pamoja na ujenzi wa bweni la madaktari walio katika mafunzo ya vitendo.

Hospitali imeanzisha huduma ya tiba kwa njia ya mtandao ambao unawezesha madaktari bingwa nje ya nchi kutoa huduma.

Hospitali ya Rufaa ya KCMC

Hospitali ya rufaa ya KCMC inayomilikiwa na Shirika la Good Samaritan inahudumia wagonjwa kutoka katika Kanda ya Kaskazini. Hospitali ina idadi ya vitanda 550.

Hospitali imeboresha huduma za magonjwa ya mifupa, njia ya mkojo na figo (Urology), ngozi, akina mama na watoto na magonjwa pua, masikio na koo.

Wizara imetoa mashine kubwa 2 za X-ray, Ultra Sound 1, C T Scan 1 na X-ray CARM 1. Vifaa hivyo vinasaidia kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa na utoaji wa tiba sahihi. Aidha, Hospitali imeweka televisheni katika kliniki zote kwa lengo la kutoa elimu ya afya kwa wagonjwa, kupata taarifa ya matukio mbalimbali na burudani.

Hospitali imeanzisha kituo cha ushauri nasaha cha ANGAZA ili kutoa huduma za ushauri nasaha kwa wananchi. Pia, hospitali inatoa huduma za chakula bila malipo kwa wagonjwa waliolazwa.

Hospitali inashirikiana na Chuo Kikuu cha Tumaini kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali za afya. Mafunzo yanayotolewa ni pamoja na Udaktari, Uuguzi, Mazoezi ya Viungo, Utengamao, Macho, Nusu Kaputi (Anaesthesia) na Utunzaji kumbukumbu za afya. Aidha, Hospitali inaendesha Mafunzo ya Uzamili katika fani mbailimbali za afya.

Wizara imejenga kituo cha Damu Salama na jengo la huduma ya wagonjwa wa nje (OPD). Ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika wodi ya wagonjwa mahututi, Hospitali hiyo imejenga wodi ya pili. Aidha, wodi zote zimeboreshwa kwa kufanyiwa ukarabati.

Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya Elizabeth Glazier Foundation imekamilisha ujenzi wa kituo cha watoto wenye maambukizi ya UKIMWI.

Hospitali ya Rufaa ya Mbeya

Hospitali ya Rufaa Mbeya chini ya Wizara inatoa huduma za kibingwa za tiba na ushauri kwa wagonjwa kutoka Mikoa ya Nyanda za Juu na Nyanda za Juu Kusini. Aidha, Hospitali hiyo inatoa mafunzo mbalimbali ya fani za afya na utafiti.

Wizara imekamilisha ukarabati wa hospitali ya wazazi Meta, jengo la utawala, majengo 6 ya wodi, karakana, sehemu ya kuegesha magari na uzio wa hosteli ya madaktari waliopo mafunzo kazini. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa vya wodi ya wagonjwa mahututi. Pia, Wizara imenunua mashine mbili za kisasa za X-ray na mashine moja ya Ultra Sound.

Hospitali inatoa huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa ambao mfumo wao wa figo umeharibika. Aidha, Hopsitali inatoa huduma ya upasuaji wa watoto wenye vichwa vilivyojaa maji.

Idadi ya wataalam (Madaktari, Wauguzi na Wafamasia) wanaofanya mafunzo kwa vitendo imeongezeka kutoka 20 hadi 45.

Hospitali ya Mirembe na Taasisi ya Isanga

Hospitali ya Mirembe na Taasisi ya Isanga inatoa huduma ya rufaa kwa wagonjwa wa afya ya akili nchini.

Wizara imejenga Kituo cha Tiba na Utengemano kwa waathirika wa dawa za kulevya. Aidha, ukarabati wa mifumo ya maji safi na taka, na uwekaji uzio wa nje na ndani katika hospitali umekamilika. Pia wodi, ofisi za utawala na kuta za ngome zimekarabatiwa.

Taasisi ya Saratani Ocean Road
Wizara imenunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kutibu magonjwa ya saratani: mashine mbili za “Cobalt 60” zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 2, mashine mbili za “Intracavitary Unit” zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni mia mbili, “Simulator”, na “Treatment Planning Unit” vyenye thamani ya shilingi milioni 280 na mashine mbili za “Gamma Cameras” ambazo zilighariimu serikali jumla ya shilingi milioni 800.

Kwa wastani wagonjwa 3,100 kwa mwaka wenye aina mbalimbali za magonjwa ya saratani, hupata matibabu. Aidha, Hospitali inatoa huduma ya Saratani ya Shingo ya kizazi kwa wagonjwa 1000 kwa mwaka na wagonjwa wengine wapya 2,100. Pia, wagonjwa wa marudio wapatao 6000 kwa mwaka hupatiwa matibabu.

Vifaa vya msaada vyenye thamani ya shilingi milioni 800 vilipokelewa kutoka“International Atomic Energy Agency - IAEA” ambavyo vinasaidia kuboresha huduma za tiba ya mionzi,aidha Serikali imechangia shiling milion 900 kwa ajili ya huduma hii.

Mradi wa kuboresha huduma za tiba ya mionzi (Improvement of Radiotherapy Services Project) ulianzishwa katika hospitali hii. Mradi huu umekuwa ukitekelezwa na serikali ya Tanzania kwa kuchangia shilingi milioni 900 pamoja na “International Atomic Energy Agency - IAEA” kwa kutoa vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 800. Mradi huu unawasaidia sana wagonjwa wa saratani katika kiwango cha hali ya juu.

Mafunzo ya kutoa matibabu ya Saratani yameanzishwa katika Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi ya Afya (MUHAS). Aidha, Mkakati wa Taifa wa kutoa huduma za saratani umekamilika na umeanza kutumika.

Hospitali ya Kibong’oto
Hospitali inatoa huduma za uchunguzi na matibabu ya magonjwa ya kifua kikuu. Wagonjwa wanaolazwa ni wale wanaoletwa kutoka hospitali za mikoa na wale wanaokuja kutibiwa bila rufaa.

Wizara imekarabati majengo ili kuboresha huduma kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu na kufuatilia mwenendo wa vimelea sugu. Aidha, majokofu mapya mawili yenye uwezo wa kuhifadhi maiti sita katika chumba cha kuhifadhia maiti yamenunuliwa kwa gharama ya shilingi milioni 30. Pia, chumba cha kuhifadhia maiti kimefanyiwa upanuzi.

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)
Taasisi imeanzisha mafunzo ya shahada ya uzamili katika fani ya mifupa (M.Med. Orthopaedic na Traumatology) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Jamii Muhimbili.

MOI imeanzisha ushirikiano na taasisi za vyuo vikuu sita nchini Marekani vya Medical University of South Carolina, University of Colorado, Weill Cornell Medical College, University of New York, Havard University na Barrow Institute of Neurology. Kutokana na ushirikiano huo, MOI imefaidika na msaada wa vifaa vya upasuaji wa uti wa mgongo vyenye thamani ya shilingi milioni 500, hadubini kwa ajili ya upasuaji yenye thamani ya shilingi milioni 200 na Endoscopic set ya shilingi milioni 300. Aidha, uhusiano huo utahusisha ubadilishanaji wa wataalamu na mafunzo kati ya MOI na taasisi hizo.

Huduma za fani ya mifupa, upasuaji wa ubongo na mifumo ya fahamu zimeboreshwa. Idadi ya wagonjwa waliopata huduma hizi kuanzia 2005, jumla ya wagonjwa 183 wamefanyiwa upasuaji wa kuweka nyonga bandia, 39 wamefanyiwa upasuaji wa kuwekewa goti bandia na upasuaji wa uti wa mgongo wagonjwa 128.

Mwaka	**2006**	**2007**	**2008**
Mahudhurio ya wagonjwa wa nje	26,425	32,128	37,471
Wagonjwa walio lazwa	4,342	5,237	5,297
Upasuaji	2,576	3,087	3,396
Upasuaji Maalum:			
▪ Nyonga	22	79	82
▪ Goti	-	-	39
▪ Uti wa mgongo	-	97	31
▪ Ubongo	52	85	94
Mazoezi ya viungo	13,536	15,339	30,049
Viungo bandia	516	699	838

WAKALA

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)

Kanuni, miongozo na taratibu za udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba zimeandaliwa na kuboreshwa ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003.

Mkataba wa Huduma kwa Wateja ulitayarishwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuweka viwango vya ubora wa utoaji huduma.

Toleo la kwanza la kitabu cha taarifa za dawa (Tanzania National Formulary – TNF) imefanyiwa mapitio. Kitabu hiki kinatumika kama rejea kwa watoa dawa katika ngazi zote.

Vipindi vya redio 28, matangazo mafupi 17 ya redio, vipindi 6 vya televisheni na mchezo mmoja wa kuigiza wa televisheni vilirushwa katika vituo mbalimbali kwa lengo la kuelimisha umma juu ya ubora, usalama na matumizi sahihi ya dawa, vyakula vipodozi na vifaa tiba. Aidha , taarifa kwa umma 49 kuhusu udhibiti wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba zilitolewa kwa umma.

Katika kufuatilia ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, sampuli 1,546 zilichukuliwa kutoka sokoni na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara ambapo sampuli 1,274 zilikidhi viwango. Aidha, jumla ya kesi 33 zinazohusiana na ukiukwaji wa Sheria ya Chakula, Dawa, na Vipodozi ya mwaka 2003, zilifikishwa katika vyombo vya dola ikiwa ni pamoja na mahakama.

Katika kuimarisha mapambano dhidi ya bidhaa bandia za chakula, dawa na vipodozi, Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa kushirikiana na jeshi la Polisi imeanzisha Kikosi kazi cha kupambana na bidhaa hizo. Aidha Opersheni maalumu ya kukamata dawa bandia ijulikanayo kama “Operesheni Mamba” ilifanyika katika kipindi hiki kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, INTERPOL, Tume ya Ushindani wa Kibiashara (FCC), Bohari ya Dawa, Mamlaka ya Mapato na Shirika la Viwango Tanzania.

Mamlaka imekamilisha mradi wa ujenzi wa ofisi mpya za Makao Makuu na kuizindua rasmi tarehe 1 Julai 2008.Aidha, ofisi tatu za Kanda za Mamlaka ya Chakula na Dawa zilifunguliwa katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Mbeya ili kuimarisha na kupeleka huduma za udhibiti karibu zaidi na wananchi.

Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu umetekelezwa kwa kushirikisha sekta binafsi na Halmashauri kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa dawa muhimu na huduma bora za dawa katika maeneo ya vijijini na miji midogo. Hadi sasa mpango huo umeenezwa katika mikoa ya Ruvuma, Morogoro, Mtwara na Rukwa.

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina uwezo wa kufanya uchunguzi na kutoa matokeo kuhusu uhalali wa mtoto kwa mzazi wa kiume, watoto wanaozaliwa na jinsia mbili ili kutambua jinsia iliyo na nguvu , magonjwa ya kurithi, ubakaji, ujambazi na mauaji kwa kutumia mtambo wa vinasaba (DNA).

Tanzania imepata zawadi ya mshindi wa kwanza mwaka 2008 ya ubunifu katika Utumishi wa Umma Barani Afrika (All Africa Public Sector Innovation Award.) kutokana na Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kusimamia vizuri matumizi ya kemikali nchini.

Maabara mbili za Mkemia Mkuu zimeanzishwa katika kanda ya Ziwa jijini Mwanza na Kanda ya Kaskazini katika Manispaa ya Arusha. Lengo ni kuharakisha utoaji huduma bora na ushauri wa kitaalam kwa wakati na kupunguza gharama ya kufuata matokeo ya uchunguzi Makao Makuu. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo jipya la Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Wizara imenunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwezesha kufanya uchunguzi. Vifaa hivyo ni pamoja na:

i. Gas Chromatography Mass Spectrometer (GC/MS) kwa ajili ya uchunguzi wa dawa za kulevya na viuatilifu

ii. Ultra Violet Visible Near Infra Red (UV/VIS-NIR) kwa ajili ya uchunguzi wa dawa zikiwemo za asili.

iii. Elemental Analyser 3100 kwa ajili ya uchunguzi wa sulphur na Nitrogen kwenye mafuta ya magari na mitambo.

Wizara imeimarisha uhusiano wa Kimataifa katika usimamizi wa kemikali kupitia mradi wa Strategic Approach on International Chemical Management (SAICM).

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeshiriki katika kikosi kazi cha kutambua watuhumiwa wa wauwaji wa watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino) na vikongwe kanda ya ziwa kwa kutumia teknolojia ya DNA.

Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali imeimarisha udhibiti wa uingizaji na usafirishaji wa kemikali hatari ya Sodium Cyanide kwenda kwenye migodi ya madini. Aidha, imeimarisha usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani.

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepata kiwanja cha kujenga Maabara ya Mkemia Mkuu Jiji la Mbeya kwa ajili ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Usambazaji wa Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba - Bohari ya Dawa (MSD)
Bohari ya Dawa imeandaa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati (Medium Term Strategic Plan 2007-2013). Mpango huu unadhamiria kuimarisha mfumo mzima wa usambazaji dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma. Kwa sasa Bohari ya Dawa ina Bohari za Kanda 8.

Usambazaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba katika hospitali, vituo vya afya na zahanati za umma umeongezeka kutoka asilimia 55 hadi 70 katika kipindi cha miaka mitatu (2006-2009). Aidha, Bohari ya Dawa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa wameanzisha ufuatiliaji wa ubora wa dawa na vifaa. Pia, Bohari ya Dawa inafanya mikutano na wadau wakiwemo wateja wote nchini. Mikutano hiyo inalenga kuwaelimisha wadau na watoa huduma juu ya taratibu za usambazaji dawa na vifaa.

Mfumo wa ugavi kulingana na mahitaji ya vituo na mgawo wa fedha (Integrated Logistics System) umeanzishwa na tayari unatumika katika mikoa 18. Ili kuboresha usambazaji wa dawa na vifaa Bohari za Kanda zimeanza

kufungasha mahitaji ya wateja katika maeneo yake badala ya kufanyika Makao Makuu Dar es Salaam.

Bohari ya Dawa imeongeza uwezo wa kuhifadhi dawa na vifaa katika maghala kutoka mita za mraba 7,565 mwaka 1994 hadi kufikia mita za mraba 30,656.

Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania

Kudhibiti upungufu wa madini joto

Tatizo la upungufu wa madini joto mwilini limeendelea kupungua kutokana na kuwajengea uwezo wazalishaji chumvi wakubwa na wadogo kuweza kuongeza madini joto kwenye chumvi wanayozalisha.

Wazalishaji chumvi wa kati na wakubwa 15 na wazalishaji wadogo 6,529 wamepewa kilo 9,000 za madini joto, pampu 4,800 za kunyunyizia madini joto kwenye chumvi na chupa 93,750 za kemikali za kupimia uwepo wa madini joto (Iodine test solution) kwenye chumvi.

Maabara ndogo zimeanzishwa katika wilaya za Tanga, Bagamoyo, Kinondoni, Kilwa, Lindi na Mtwara ili kupima viwango vya madini joto iliyopo kwenye chumvi inayozalishwa katika maeneo hayo.

Asilimia 83 ya kaya nchini zinatumia chumvi yenye madini joto na ongezeko la uvimbe wa tezi la shingo limedhibitiwa. Hivi sasa ni asilimia saba (7) tu ya Watanzania wenye tatizo hilo.

Udhibiti wa upungufu wa vitamini A

Matone ya vitamini A na dawa za minyoo zinatolewa mara mbili kila mwaka kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika wilaya zote za Tanzania Bara. Zaidi ya asilimia 90 ya watoto waliolengwa walipatiwa huduma hizi.

Utoaji wa matone ya vitamini A unafanyika sanjari na uhamasishaji wa uzalishaji, hifadhi salama na ulaji wa vyakula vyenye vitamini A na madini kwa wingi katika jitihada za kukabiliana na tatizo la upungufu wa vitamini A nchini.

Kuboresha unyonyeshaji na ulishaji wa watoto wadogo

Watoa huduma 100 wamepata mafunzo kuhusu unyonyeshaji na ulishaji wa watoto wachanga na wadogo yanayojumuisha ushauri nasaha kuhusu unyonyeshaji na ulishaji wa watoto wachanga na wadogo na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Sheria ndogo inayosimamia uuzaji na usambazaji wa maziwa mbadala na vyakula vya watoto wachanga ya mwaka 1994 ilidurusiwa ili kuboresha usimamiaji wa uuzaji wa vyakula hivyo kuimarisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama na kuendeleza lishe ya watoto wachanga.

Hospitali 68 zimefanikiwa kuwa Hospitali Rafiki za Mama na Mtoto zinazolenga kuboresha hali ya afya na lishe ya watoto nchini.

Lishe na UKIMWI

Watoa huduma majumbani na watoa ushauri nasaha 688 katika wilaya 39 za Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Mbeya, Rukwa na Iringa wamepata mafunzo kuhusu lishe kwa wagonjwa wa UKIMWI. Aidha, wakufunzi 111 kutoka vyuo vya ualimu 37 walipewa mafunzo kuhusu UKIMWI na Lishe.

Nakala 17,000 za mwongozo wa kitaifa kuhusu lishe bora kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI, zimechapishwa na kusambazwa kwenye hospitali, Vyuo vya Afya na Taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI.

Utafiti wa chakula kinachofaa kuongeza virutubishi vya vitamini na madini kwa ajili ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI umefanyika. Tafiti hii imeonyesha Chakula hiki ambacho kinatokana na mazao yanayopatikana hapa nchini kimeonyesha uwezo wa kuboresha Afya ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI. Chakula hiki kinatokana na mchanganyiko wa unga wa mahindi, soya pamoja na virutubishi vya madini na vitamini ambavyo vyote vinapatikana humu humu nchini. Matokeo ya awali yameonyesha kuwa afya ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI waliotumia chakula hiki imeimarika.

Uenezaji wa Teknolojia ya Usindikaji Bora wa Unga wa Muhogo na Vyakula vya Watoto

Wakulima 127 wa muhogo katika wilaya zinazolima kwa wingi zao la muhogo za Rufiji, Newala, Kigoma, Kibondo, Kasulu na Kibaha wamepata mafunzo ya uhifadhi, usindikaji na matumzi ya zao la muhogo. Mafunzo haya yalilenga kuongeza ubora wa zao la muhogo na unga wa muhogo.

Wakufunzi 130 katika Halmashauri za Manispaa 12 za Tanga, Moshi, Arusha, Ilala, Kinondoni, Temeke, Mbeya, Iringa, Songea, Musoma, Ilemela na Nyamagana wamepata mafunzo yanayohusu ubora na usalama wa vyakula vya watoto na teknolojia asili za kuboresha vyakula hivyo.

Elimu ya Lishe kwa Wanahabari

Wahariri 10 na waandishi wa habari 22 kutoka vyombo mbalimbali vya utangazaji vya Umma na binafsi wamepata mafunzo ya ukusanyaji na utoaji wa habari na taarifa za lishe ili kuchangia katika kueneza elimu ya lishe kwa jamii.

Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

Wizara imekamilisha ujenzi wa ofisi mpya ya Makao Makuu ya Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu Dar es salaam. Maabara mpya na ya kisasa ya kuratibu na kutoa mafunzo ya viwango na ubora wa maabara nchini (Quality assurance and Training Laboratory) imeanzishwa. Aidha, ukarabati wa

maabara za Mbeya, Hospitali ya Bombo,Tanga, Hospitali ya Wilaya ya Korogwe na Kituo kipya cha utafiti wa dawa asilia cha Ngongongare, Arusha umekamilika.

Utafiti wa chanjo dhidi ya malaria umefanyika katika Wilaya ya Korogwe. Utafiti wa awali unaonyesha kuwa chanjo hiyo inaweza kukinga watoto dhidi ya malaria kwa asilimia 56.

Taasisi ya utafiti wa magonjwa ya binadamu imekamilisha mkakati wa huduma za afya kwa kuhakikisha kuwa kila inapofanya utafiti katika hospitali inanunua vifaa vya kisasa vya maabara na ICT na kuviacha viendelee kutumika katika hospitali hizo hadi sasa vifaa hivyo vipo katika hospitali ya Wilaya Kilosa, Haydom na Korogwe.

Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu imeandaa Mpango wa Miaka Mitano, (NIMR Strategic Plan 2008 –2013).

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NIHF)

Idadi ya watanzania wanaohudumiwa na Mfuko huu imeongezeka kutoka wanachama 1,152,995 (asilimia 3.4 ya watanzania) mwaka 2004/05 hadi kufikia 1,809,671 mwezi Desemba 2008 (asilimia 5.3 ya watanzania). Lengo ni kuwafikia asilimia 45 ya watanzania wote ifikikapo mwaka 2015.

Kitita cha mafao kimeboreshwa na kinachojumuisha ongezeko la dawa 110 katika orodha ya awali ya dawa 445 ya mwaka 2005 na kufikia aina 555 mwaka 2008, ambazo zinatibu magonjwa yote ukiacha yale yaliyo katika mpango wa Serikali.

Huduma za vipimo na uchunguzi wa maabara zimeongezeka kutoka vipimo 54 mwaka 2005 hadi kufikia vipimo 137 mwaka 2008. Aidha, huduma za mafao ya miwani ya kusomea kwa wanachama wachangiaji zilianza kutolewa kuanzia mwezi Februari 2006.

Maduka ya dawa muhimu vijijini yapatayo 122 yamesajiliwa na Mfuko hadi Machi 2009 katika Mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Mtwara na Rukwa. Maduka hayo yamesaidia upatikanaji wa huduma ya dawa kwa wanachama hasa maeneo ya vijijini.

Katika kipindi cha 2007 hadi Machi 2009 mikopo nafuu ya vifaa vya hospitali vyenye thamani ya shilingi milioni 848.4 ilitolewa kwa vituo 45 vya kutolea huduma za afya katika mikoa 13 ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Mwaza, Rukwa, Dodoma, Mtwara, Mbeya, Kagera, Mara, Kilimanjaro, Singida na Tabora. Aidha, mikopo kwa ajili ya ukarabati ya shilingi milioni 380.4 ilitolewa kwa vituo 9 vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Mara, Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Kagera, Mbeya na Ruvuma.

Mfuko umekarabati Kliniki ya Ocean Road ya Jijini Dar es salaam inayotoa huduma kwa wanachama na wananchi kwa ujumla jijini. Aidha, mafao ya matibabu kwa wanachama wastaafu yataanza rasmi mwezi Julai 2009.

Hitimisho

Kutokana na mikakati mbalimbali iliyopo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Katika kipindi cha miaka mitatu huduma nyingi zimeboreshwa na mafanikio yamepatikana hivyo kupunguza maradhi na vifo vya jamii ya watanzania.

Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia kanuni na taratibu zote za utoaji wa huduma za sekta ya afya na ustawi wa jamii nchini, ambapo wafanyakazi wameendelea kutoa huduma kwa juhudi kubwa na mafanikio ya juu. Aidha, Wizara imeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Vikao vya makatibu wakuu ambapo masuala ya sekta nyingine zenye uhusiano na sekta ya afya na ustawi wa jamii na kuwezesha sekta ya afya kuendelea kupata kipaumbele katika bajeti na kuwa ya tatu.

ii. Vikao vya majadiliano na wadau wa maendeleo wa sekta ya afya pamoja na kushiriki vikao vya aina hiyo katika ngazi ya kitaifa ambapo sekta ya afya imeendelea kuungwa mkono na kuendelea kupata misaada.

iii. Ziara za kutembelea watendaji katika mikoa ya, Morogoro, Mwanza, Arusha, Mara, Tabora, Dar es Salaam na Tanga na pia katika ziara za Mheshimiwa Rais katika mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga na Dodoma.

iv. Vikao vya bodi ya ushauri ya ECSA health ambapo Tanzania ni Mwenyekiti, Visiwa vya Shelisheli na Arusha Tanzania, ambapo masuala mbalimbali ya afya kikanda yalijadiliwa.

Mafanikio mengi ya utekelezaji yamepatikana kutokana na kuwasilisha wadau wa Sekta ya Afya katika utekelezaji wa kazi zote, kwani kila mwananchi ana mchango mkubwa sana katika kulinda na kutunza afya yake, ya familia yake, jamii na Taifa zima kwa ujumla. Hivyo, wizara itaendelea kuwashirikisha wadau wote katika utekelezaji/utoaji wa huduma za Afya.